# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bon*

Toleo Nambari 07 | Oktoba 16, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO






# MRITHI MATATA

**Akiwa msimamizi mkuu wa shughuli za Raila katika uchaguzi wa Agosti 9, Winnie Odinga alikuwa na uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu kampeni za Azimio La Umoja, akikwaza wengi kwa ushupavu wake. Lakini je, mwanamke huyu mchanga anatosha kurithi himaya ya kisiasa ya baba yake?**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

## anywhere, anytime.




Follow the link to subscribe

> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play

Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111
Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyomo

**5 KITENDAWILI CHA MASHOGA:** Kutetea jamii ya mashoga Kenya kuishi bila vitisho kumekuwa kukifanywa kwa minong'ono na kumepata hasara zaidi ya ufanisi, hata baada ya kupitishwa kwa katiba ya 2010.

**13 MITINDO:** Kutoka kwa kuwavisha watu maarufu na wanasiasa matajiri hadi wanahabari, chapa ya mavazi ya Beverly Mawia Muthengi, Africa Yuva - Nyumba ya Mitindo ya Kiafrika - inaimarisha ubunifu wa mavazi kwa kiwango kipya kabisa.

**22 ULIMI MWEPESI:** Kuropokwa kwa Rigathi Gachagua na matamshi yake ya umma yasiyopangwa mwishowe kunaweza kumsawiri kama mwanasiasa asiyeweza kuaminika.



**30 KICHEKO CHA MWISHO CHA CHEPKUT:** Ucheshi wa mbunge wa zamani na unyenyekevu wake haukuwa wa kutafuta umaarufu wa kisiasa lakini ulihusu kutangamana na wananchi wa kawaida ambao walikuwa wamempa nafasi ya kuwahudumia.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

# Mwisho wa vita dhidi ya ufisadi



**Mutuma Mathiu**

**Ufisadi nchini Kenya ni nanga ya nguvu za kisiasa. Kampeni za uchaguzi huendeshwa kwa pesa za umma zilizoporwa; ni utajiri wa Wakenya wachache ambao haujapatikana kwa ufisadi. Kufaulu kwa vita dhidi ya ufisadi kunaweza kupatikana tu kutokana na kubadilisha siasa, sio kuziendeleza.**

Katika muhula wake wa pili, Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta alianzisha kampeni dhidi ya ufisadi na akaunda kundi la kuitekeleza. Wasiopendezwa walisema mpango huo ulikuwa njama ya kummaliza Naibu Rais William Ruto kwa kulenga biashara zake na za washirika wake katika mashirika ya serikali na maeneo mengine. Waliokuwa na matumaini walitarajia hatimaye, kuna mtu alikuwa akifanya jambo kuhusu kinachoponza Kenya: nchi ambayo ni maskini na si kwa sababu watu wake ni wavivu au wapumbavu, lakini kwa sababu ya wizi wa pesa za umma ambao umeharibu uchumi na kuukausha kabisa.

Katika vita vyake, Bw Kenyatta aliunda kundi la watu waaminifu, baadhi walioweza kuonekana hadharani ilhali wengine walikuwa wamefichwa ndani kabisa ya iliyoitwa Deep State.

Bw Noordin Haji aliteuliwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, Bw Goerge Kinoti Mkuu wa Idara ya Uchunguzi wa Uhalifu, Jaji Mstaafu Kihara Kariuki akateuliwa Mwanasheria Mkuu na Meja (mstaafu) Twalib Mbarak akateuliwa Afisa Mkuu Mtendaji wa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi, miongoni mwa wengine. Nyuma yao kulikuwa na wengine wenye nguvu kusaidia kampeni dhidi ya ufisadi.

Ni Bw Kinoti na Bw Haji walioibuka kuwa maarufu katika vita hivi.

Walikuwa wamefanya kazi kwa miaka mingi katika utekelezaji wa sheria na bidii na imani zao zilipendeza.

Kutofautiana kwa wawili hao, na kufanya vigumu zaidi kwa mashirika yao - Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (ODPP) na Idara ya Uchunguzi wa Uhalifu (DCI) - kushirikiana, kumejadiliwa na kuripotiwa kwa miezi kadhaa.

ODPP ililaumu DCI kwa kufanya uchunguzi duni na kuwasilisha ushahidi ambao haungeweza kufanikisha mashtaka, huku DCI ikidai ina haki za kushtaki na kulaumu ODPP kwa kuingiza siasa na kujikokota kushtaki washukiwa.

Kuondolewa ghafla kwa kesi za ufisadi na DPP siku za hivi majuzi na kujiuzulu kwa Bw Kinoti kulithibitisha kutojitolea kwa Kenya katika vita dhidi ya ufisadi na kunaashiria kuporomoka kwa kampeni ya Bw Kenyatta, iwe ilikuwa halisi au la.

Ufisadi nchini Kenya ndio nanga ya kisiasa. Kampeni za uchaguzi huendeshwa kwa pesa za umma zilizoporwa; ni utajiri wa Wakenya wachache ambao haukupatikana kwa ufisadi.

Kufaulu kwa vita dhidi ya ufisadi kunaweza kupatikana tu kutokana na kubadilisha siasa, sio kuziendeleza. Kwa kuweka presha kwa Bw Haji kutoa sababu za kina za kuondoa kesi za ufisadi, Chama cha Mawakili Kenya kimempa DPP kitendawili kigumu kutegua: Je, ofisi huru ya kikatiba ilikubali kufungua mashtaka katika kesi zilizo na dosari? Kama ndivyo, kwa nini na ni wakati gani dosari hizo ziligunduliwa na ni hatua gani zilichukuliwa kuzirekebisha?

Jinsi ODPP itashughulikia hili itaamua iwapo wananchi wataendelea kuamini na kusaidia vita dhidi ya ufisadi au watakosa matumaini na kukosa kuamini juhudi hizi siku zijazo. Kwa vyovyote vile, na hata kama haikubaliki kushtaki mtu bila ushahidi wa kutosha, kuporomoka kwa kesi hizo hakutasaidia kampeni siku zijazo.

Hatima ya wanaochunguza kesi zinazomkabili Naibu Rais Rigathi Gachagua kwa hakika lazima inawafanya wanaochunguza ufisadi kuhofia usalama wao.

Hawakunufaika na mchakato unaofaa kufuatwa na hakuna uhakika ilizingatiwa kwamba walikuwa wamepewa maagizo. Afisa wa upelelelezi anayeagizwa kuchunguza kesi inayohusu mtu mwenye nguvu siku zijazo atakuwa akijitahidi sana kuepuka majaribu ya kutoroka.

Hii ni wiki mbaya kwa vita dhidi ya ufisadi.

*mmutuma@ke.nationmedia.com*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Darubini Ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno


**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Mutuma Mathiu** Mhariri Mkuu
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Wabunge kuanza shughuli wiki hii


# Maandalizi ya kuwapiga msasa mawaziri walioteuliwa tayari

Kupigwa msasa kwa walioteuliwa mawaziri kunaanza Jumatatu. Shughuli hiyo itaendeshwa na Kamati ya Bunge ya Taifa Kuhusu Uteuzi. Wanachama wa kamati hiyo ni Nelson Koech, Rahab Wachira Mukami, Dido Ali Raso, George Murugara, David Gikaria, Ferdinand Wanyonyi, Mary Emaase, Abdul Rahim Dawood, Junet Mohammed, Caleb Amisi, Stephen Mule, Abdi Shurie, Naisula Lessuda, David Pkosing na Mishi Mboko.
Kamati hiyo inatarajiwa kuthibitisha uwezo na kuhitimu kwa walioteuliwa kuhudumu katika ofisi ya umma kulingana na Sura ya Sita ya Katiba. Pia itachunguza kuidhinishwa kwa walioteuliwa na idara tofauti, ikiwemo Idara ya Uchunguzi wa Uhalifu, Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi, Mamlaka ya Ushuru na Bodi ya Mikopo ya Masomo ya Elimu ya Juu. Wawili walioteuliwa, Mithika Linturi (Kilimo) na Aisha Jumwa (Jinsia), waliondolewa kesi za uhalifu zilizowakabili. Kesi ya Jumwa alihusu ufisadi na ya Linturi ilihusu ubakaji.




Rais William Ruto na Mkuu wa Utumishi wa Umma Joseph Kinyua katika Ikulu ya Nairobi mnamo Septemba 27 alipotangaza baraza lake la mawaziri. Anayengalia ni Waziri Mkuu mteule Musalia Mudavadi.

■ Kampuni zinatumia dola $44m kwa siku



Wachimbaji madini waliogoma wakiandamana mjini Marikana, kilomita 40 kutoka eneo la Rustenburg, yanakopatikana madini ya platinum nchini Afrika Kusini, mnamo Mei 14, 2014. Mgomo wa muda mrefu wa wafanyakazi wa shirika la serikali linaloshughulikia uchukuzi wa madini la Transnet umeathiri bandari na reli na kuumiza uchumi. PICHA | AFP

# Mgomo wa wahudumu wa bandari na reli waumiza uchumi wa Afrika Kusini

Serikali ya Afrika Kusini wiki hii ilisema "inatiwa wasiwasi" sana na mgomo uliochukua siku nyingi katika kampuni inayomilikiwa na serikali ya Transnet, ambao umeathiri bandari na reli, kuzuia bidhaa kuuzwa nje na kuumiza uchumi.
Wafanyakazi wa kampuni hiyo, inayosimamia mtandao wa uchukuzi wa reli na bandari zote katika nchi iliyo na uchumi mkubwa wa viwanda Afrika, waligoma wiki jana wakitaka waongezwe mshahara huku mfumko ukizidi kupanda.
"Serikali ina wasiwasi mwingi kuhusu athari mbaya kwa uchumi wa Afrika Kusini," mawaziri wa Afrika Kusini wa Leba, Kilimo na Biashara za Umma wakasema katika taarifa ya pamoja.
Waliomba kurudiwa "haraka iwezekanavyo" kwa uuzaji nje wa bidhaa za kilimo, madini na zingine wakisema zinachangia kudumisha maelfu ya kazi kote nchini humo.
Mgomo huo unagharimu kampuni za kuchimba madini randi 815 milioni (dola 44 milioni za Amerika 44) kila siku, kulingana na Baraza la Madini la Afrika Kusini, ambalo ni kundi la viwanda.
Bandari za kupeleka madini nje ya nchi zinahudumu kwa kati ya asilimia 12 na 30 ya uwezo wake siku moja, kundi hilo lilisema katika taarifa, na kuongeza kuwa "hii inaharibu uchumi ambao tayari umedorora".

■ Duru zahofia kuzungumza na wanahabari

# Spyware ni tisho kwa wanahabari




Programu za kisasa za ujasusi ni tishio "halisi" kwa wanahabari wapekuzi, na kufanya duru kuogopa kuzungumza kwa hofu ya kutambuliwa, shirika la kutetea wanahabari la Amerika limeonya. Likikubaliana na mashirika kadhaa yasiyo ya kiserikali, Committee to Protect Journalists lilihimiza kusimamishwa mara moja kwa utengenezaji, uuzaji na matumizi ya programu hiyo hadi kuwe na hakikisho kuwa wanahabari wanalindwa. "Najua kwa kweli kuwa watu wengi wanaogopa kuzungumza na mimi. Watu wengi wanaogopa kuniandikia, wanahofia simu yangu inachungunzwa," akasema mwanahabari wa Morocco, Aida Alami, anayefanya kazi na New York Times.

■ Uvumbuzi nadra kwa kiwango cha ulimwengu

# Mchoro 'adimu' wa Kirumi wapatikana



Mchoro uliotengenezwa miaka 1,600 iliyopita, enzi za utawala wa Warumi, ambao haukuwa umeharibika, umevumbuliwa Syria ya Kati. Mchoro huo wenye ukubwa wa mita 20 x 6m (futi 65.5 x 20), ulipatikana chini ya jengo eneo la Rastan karibu na Homs, mji ambao ulikuwa umetekwa na waasi wakati wa vita vya ndani hadi mwaka wa 2018.
Mchoro huo unaonyesha matukio, yakiwemo ya vita vya Trojan na Amazon, unasemekana kuwa nadra sana wa aina yake.
Hazina nyingi za akiolojia za Syria ziliharibiwa baada ya vita vya zaidi ya mwongo mmoja. Lakini uvumbuzi wa hivi punde unatajwa kuwa muhimu zaidi wa akiolojia tangu mwanzo wa mzozo huo mwaka wa 2011. "Kilicho mbele yetu ni uvumbuzi nadra kwa kiwango cha ulimwengu," Hamman Saad, afisa mkuu wa Idara ya Makavazi na Sanaa ya Syria, akaambia AP

*- Zimetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ MJADALA MKALI KUHUSU LGBTQ

# KITENDAWILI CHA MASHOGA

*Kampeni za kutetea mashoga jamii ya mashoga nchini Kenya kuishi kuishi maisha yao bila vitisho, dhuluma, ghasia, ubaguzi na sheria kandamizi zimekuwa zikiendeshwa kwa minong'ono, na mara nyingi zinapata pigo badala ya ufanisi hata baada ya kupitishwa kwa katiba ya 2010. Mara nyingi, kampeni za haki za mashoga huchukuliwa kuwa ajenda inayosukumwa na wageni. Hali hii itabadilika huku wengi wakijitokeza?*



• Na MACHARIA GAITHO

Kampeni za kupigania haki za binadamu, chaguo la kisiasa, uhuru wa kujieleza na haki zingine za kimsingi zimepiganiwa kwa wazi na kwa sauti kubwa kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita, na kupata ufanisi mkubwa tangu enzi za utawala wa kidikteta wa chama kimoja.

Katika kipindi hicho, hata hivyo, kampeni za kutetea mashoga kuishi bila vitisho, dhuluma, ghasia, ubaguzi na sheria kandamizi zimekuwa zikiendeshwa kwa minong'ono, na mara nyingi zinapata pigo badala ya ufanisi hata baada ya kupitishwa kwa katiba ya 2010.

Mara nyingi, kampeni za haki za mashoga huchukuliwa kuwa ajenda inayosukumwa na wageni. Hili linashuhudiwa kila wakati CNN na mashirika mengine ya habari Ulaya na Amerika yakihoji rais wa Kenya, au rais wa Amerika au balozi wake anapogusia masuala ya Kenya.

Mtangazaji maarufu wa CNN, Christianne Amanpour, alifuata mkondo huo alipomhoji Rais William Ruto mnamo Septemba 7.

Ilivyotarajiwa, aliuliza kuhusu madai ya ukandamizwaji wa mashoga Kenya, na Rais alitoa jibu lililokuwa limefikiriwa vyema: "Ninasema wazi kuwa tunaheshimu kila mtu na wanachoamini, lakini pia tuna tunachoamini na tunatarajia tuheshimiwe kwa kile tunachoamini," alijibu.

"Hatutaki kufanya mambo madogo kuwa makubwa…. litakapokuwa suala kubwa kwa watu wa Kenya, watu wa Kenya, watafanya uamuzi," akahitimisha.

Jibu la Ruto lilifanana na la mtangulizi wake, Rais Uhuru Kenyatta, ambaye aliambia Amanpour mnamo 2018: "Ninataka kueleweka wazi, sitazungumzia suala ambalo halina umuhimu wowote kwa watu na Jamhuri ya Kenya. Huyu si Uhuru Kenyatta anayesema ndiyo au la, hili ni suala ambalo watu wa Kenya wamejiwekea wenyewe katika katiba baada ya miaka mingi na wakasema wazi kuwa si suala wanalotaka kuzungumzia wakati huu.

"Katika miaka ijayo, pengine miaka mingi baada ya mimi kuwa rais, nani anayejua?" Pengine jamii yetu itakuwa imefikia wakati ambao hayo ndiyo masuala watu watakuwa wakitaka kuzungumzia wazi na kwa njia huru".

Alitamatisha kwa kusema kuwa yuko na maoni yake ya kibinafsi kuhusu suala hilo, lakini hangeyatoa kwa sababu akiwa rais, anafaa kuzungumzia yale watu wa Kenya waliamua kuweka katika sheria.

Kimsingi, Ruto na Uhuru walikataa kusema iwapo watatambua haki za mashoga, kwa kujificha katika mazingira ya kitamaduni na kidini ambapo suala hilo ni mwiko; na sheria ambazo zinarahamisha ngono na ndoa kati ya watu wa jinsia moja.

Hata hivyo, ilionekana kuwa, tofauti na, kwa mfano, Rais Yoweri Museveni wa Uganda au aliyekuwa rais wa Zimbabwe, Robert Mugabe, hakuna kati ya Ruto na Uhuru aliyelaani wazi mapenzi ya watu wa jinsia moja.

Wote waliacha nafasi ya mazungumzo wakati fulani siku zijazo wakati watu wa Kenya watakuwa tayari kukabiliana na suala hilo.

Hali kwambakatika mahojiano yote mawili hakuna aliyelaani mtindo wa maisha wa mashoga na pia kwamba kulikuwa na nafasi ndogo sana iliyoachwa kwa mazungumzo siku zijazo, inaweza kuchukuliwa kuwa chan-

...Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Jamii ya mashoga yajitokeza

...Kutoka Uk 5

ya, lakini si kwa wanaotambua kukataa kutetea sehemu ya raia wanaokabiliwa na ubaguzi, vitisho, ghasia na kunyimwa haki za kimsingi za kikatiba za kuishi na uhuru.

Jamii ya mashoga, ambayo iliamua kutambuliwa kwa herufi ndefu LGBTQ (Wasagaji, Mashoga, walio na jinsia mbili na waliobadilisha jinsia) inasisitiza kuwa kuna masuala yasiyofaa kufichwa.

Kuna vizingiti vya kisheria na kikatiba dhidi ya ngono na ndoa za watu wa jinsia moja. Kisha kuna maadili ya kijamii katika nchi inayokumbatia imani za kitamaduni na kidini (Ukristo na Uislamu) ambazo zinakataa kabisa mahusiano ya kimapenzi ya watu wa jinsia moja.

Kuhusu mahojiano ya CNN yaliyoachana kwa miaka minne, Bi Njeru Gateru, mkurugenzi mkuu wa Muungano wa Kitaifa wa Haki za Mashoga na Wasagaji (NGLHRC) hakufurahia kamwe. "Inasikitisha kwamba walio mamlakani wanachukulia masuala ya haki za binadamu kuwa yasiyofaa," akaambia Darubini ya Wiki.

"Kauliza Uhuru na Ruto ni kuwa watu wa LGBTQ waendelee kunyanyaswa kwa sababu ya chaguo lao la jinsia. Kama mtu asiyetamani ngono inatamausha kuwa kutofahamu masuala hayo kunaendelea chini ya miezi mitatu kutoka tulipolalamika hadharani kuhusu mauaji ya msagaji kwa sababu ya chaguo lake la jinsia. Dhuluma hizi zinaendelea kuongezeka bila hatua kutoka kwa serikali."

Alikuwa akimaanisha kisa cha Sheila Lumumba, 25, mfanyakazi wa hoteli mjini Karatina ambaye alibakwa na genge la wanaume na kuuawa, kitendo ambacho kilisababisha maandamano nchini na kimataifa.

Mwezi Julai, kufuatia maandamano ya siku nyingi ya jamii ya mashoga na wanaharakati wa haki za binadamu dhidi ya polisi kwa kutochukua hatua, mshukiwa mmoja alikamatwa na kushtakiwa katika mahakama ya Nyeri kwa kushambulia na kuua.

Mashirika ya haki za binadamu pia yamekuwa yakishinikiza polisi wachukue hatua haraka kuhusu mauaji ya hivi majuzi, yakiwemo ya mwanamume shoga, Joash Mosoti, aliyeuawa Mombasa mwaka jana na Rose Mbesa, mwanamume mwenye jinsia mbili aliyeuawa Kaunti ya Trans Nzoia mapema mwaka huu.

Hashitegi #JusticeForSheilaLumumba, #JusticeForRoseMbesa, #JusticeForJoashMosoti zilivuma huku wanaharakati wakiweka presha, wakisisitiza kuwa hayo hayakuwa mauaji ya 'kawaida', lakini yaliyolenga wanaokumbatia jinsia tofauti.

Ingawa jamii ya mashoga Kenya imekuwa ikibainika na kuzungumza wazi katika miaka ya hivi majuzi, wamekuwa na tahadhari tangu kuchaguliwa kwa Rais Ruto, na uhusiano wake na makundi ya kievanjelisti yasiyo na subira.

Darubini ya Wiki ilipoanza kutayarisha habari hii, wanaharakati wengi wa kutetea mashoga waliofikiwa ambao awali walikuwa wakionea fahari jinsia zao, walichagua kutozungumza na kusubiri kuona kitakachotokea.

Hofu ya kuibuka kwa utawala usiovumilia mambo fulani ilionekana kuhalalishwa wakati, bila kutarajiwa, Kaimu Afisa Mkuu Mtendaji wa Bodi ya Kutathmini Filamu Kenya (KFCB) Christopher Wambua, alipotangaza kuwa sinema zote zilizo na maudhui ya ushoga na usagaji ni marufuku Kenya.

Katika mahojiano na redio ya Spice FM mnamo Septemba 23, Wambua alifichua kuwa Bodi hiyo ilikuwa imepiga marufuku sinema kadhaa zilizotayarishiwa Kenya na ng'ambo ambazo zilikuwa na maudhui ya LGBTQ.



**Njeri Gateru** mkurugenzi mkuu wa Muungano wa Kitaifa wa Haki za Mashoga na Wasagaji.

Hakutaja sheria zilizotumiwa kupiga marufuku maudhui hayo isipokuwa sharia ambayo imekuwepo inayopinga ngono ya mashoga.

Hiyo inaonekana kuwa kutafsiri sheria kimakosa kwa makusudi, kwa kuwa, kama sheria inasema kitendo fulani ni uhalifu, haisemi kujadili au kueleza kitendo hicho ni uhalifu. Aidha, si kukiuka sheria kupigania kitu kisiwe uhalifu.

Katika kauli zake, Wambua anaonekana kufuata mantiki ya mtangulizi wake Ezekiel Mutua, aliyebandikwa majina 'Yesu Mdogo' na 'Kiranja wa Maadili' kwa kujaribu kulazimisha mwongozo wake wa maadili kwa wengine.

Ni katika muhula wa Mutua mnamo 2018 ambapo filamu iliyotayarishwa na Wakenya, 'Rafiki', ilipigwa marufuku kwa sababu ilionyesha mapenzi ya wasagaji. Ajabu ni kuwa aliondoa marufuku hiyo kwa muda ili filamu hiyo iliyoandikwa na kuelekezwa na Wanuri Kahiu, iweze kushirikishwa kama filamu ya Kenya katika Oscar Awards.

Njeri wa NGLHRC alishangazwa na kauli za Wambua, akizifananisha na kukatiza haki za kisheria na kikatiba za uhuru wa kujieleza.

Aliongeza kuwa kupiga marufuku sinema hiyo kwa sababu ilionyesha mapenzi ya watu wa jinsia moja ni sawa na jaribio la kufuta ukweli na pia kufuta habari za watu wa jamii fulani.

Darubini ya Wiki ilipowasiliana na Wambua, alionekana kuondoa taarifa yake, akikanusha kuwa alipiga marufuku filamu zinazoonyesha maudhui ya ushoga.

Alikubali kuwa hakuna sheria inayopiga marufuku maudhui ya ushoga katika filamu, lakini kuna viwango vya utathmini filamu vya bodi vinavyoongoza watayarishaji wa sinema kuhusu kinachokubalika Kenya, hasa kuhusiana na kulinda watoto na maadili ya kitamaduni.

Alisisitiza kuwa shida si maudhui ya ushoga yenyewe, lakini maudhui inayoonekana kusifu na kuinua mtindo wa maisha ya ushoga. Hapo kunaweza kuwa na shida kwa kuwa anayetathmini anaweza kutafsiri chochote kuhusu ushoga kwa muktadha huo.

*-Imetafsiriwa na Benson Matheka*

# Masaibu ya mtetezi wa mashoga

Unapomuona mara ya kwanza, Njeri Gateru anaonekana mwanamke kijana, anayejiamini na mtalaamu anayepanda ngazi katika shirika.

Lakini dakika chache za mazungumzo, mtu anaona mwanaharakati aliyejitolea kutetea wachache ambao kila siku wanabaguliwa, kutishwa na kudhulumiwa, huku maafisa wa serikali wakikosa kuchukua hatua.

Akiwa Mkurugenzi Mkuu wa Muungano wa Kitaifa wa Haki za Binadamu za Mashoga na Wasagaji, Njeri haongozi kampeni kutetea kundi linalokandamizwa pekee, bali pia anafanya hivyo kwa vitendo akiwa mmoja wa wasagaji Wakenya walio na ujasiri wa kutangaza hadharani chaguo lao la jinsia.

Nilipozungumza naye Njeri alionekana kutojua aseme nini, kisha mwenye hasira, alipoulizwa kuhusu safari yake binfasi ya kujitambua kuwa shoga.

Kwake, hilo si suala la maana. Hakuna shaka yoyote ya kutojielewa. Mapema katika maisha, alitambua kuwa alikuwa akipenda wasichana jinsi tu wenzake walipenda wavulana. Pia hakuna shida yoyote kujitokeza kwa kuwa hakuwa ameficha chaguo lake la jinsia kutoka kwa familia yake, marafiki na watu walio karibu naye. "Familia yangu inajua, imekuwa ikijua. Sijawahi kuhisi haja ya kuficha kuwa mimi ni msagaji na kwamba nawapenda wanawake," akasema. "Mahali nimekataliwa kwa sababu ya chaguo langu la jinsia ni kutoka kwa watu ambao hawanijui".

Kwa watu wengi mashoga, kujitokeza hadharani baada ya miaka mingi ya kujificha ni jambo kubwa, ni tukio la ukombozi. Kwa Njeri, hakuna chochote cha kushtuka kuhusu maisha yake ya ngono. Huwa anakabiliana na chuki karibu kila siku, hasa kwa sababu kazi yake inayohusu kusaidia waathiriwa wa unyanyasaji, dhuluma na ubaguzi.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ GWARIDE LA FAHARI: SASA SI MZAHA TENA

*Nchini Amerika, Canada na Uingereza, viongozi wanaunga mkono na kutetea haki za wasagaji, mashoga, wenye jinsia mbili na waliobadilisha jinsia*

# NCHI YA WATU HURU

• Na KWENDO OPANGA

Akiwa ameteua watu 200 zaidi kuliko utawala mwingine walio wanachama wa jamii ya wasagaji, mashoga, wenye jinsia mbili, waliobadilisha jinsia na ambao bado hawajaamua jinsia (LGBTQ), Rais Joe Biden ameinua kundi hilo la wachache ulimwenguni.

Ilikuwa hatua makusudi na ujumbe kutoka Amerika kwa sababu Biden aliahidi kuwa msaada wa kidiplomasia na wa kigeni wa Amerika "utainua na kulinda haki za binadamu za watu wasagaji, mashoga, wenye jinsia mbili na waliobadilisha jinsia kila mahali".

Na mwezi uliopita, katika ishara nyingine ya kujitolea kwake kutambua LGBTQ, Biden alitazama nje ya fuo za Amerika alipotuza mwanamuziki wa Uingereza, Elton John, anayetambuliwa kwa miaka mingi kuwa LGBTQ, na medali ya Taifa ya Sanaa. Tuzo hiyo inayotolewa kila mwaka, inatambua watu, makundi au taasisi zinazosaidia kukuza ufahamu wa taifa wa sanaa, kupanua ushirikishi wa raia katika historia, fasihi na filosofia miongoni mwa masomo mengine.

Waziri wa Uchukuzi, Pete Buttigieg, ndiye mtu wa kwanza kutangaza kuwa shoga kuhudumu katika Baraza la Mawaziri la Amerika. Mnamo Mei, Biden alimteua Karine Jean-Pierre kuwa mtu wa kwanza mweusi kutangaza kuwa shoga kuhudumu kuwa Mkuu wa Habari katika Ikulu ya White House.

Kuna uwezekano mdogo kwamba desturi hii itaigwa na Afrika hivi karibuni. Watu wa LGBTQ katika bara hili wamesikia na kuona marais wakinuna na kuwadharau na wanajua huwa wanafanyiwa mzaha.


Viongozi wa Afrika kama vile Rais wa Uganda Yoweri Museveni, tangu 2009 wamekuwa wakitofautiana na Uingereza, Amerika na Canada, kutaja tu nchi chache, kuhusu haki za jamii ya LGBTQ.

Ilianza na mbunge wa Uganda aliyewasilisha mswada wa kibinafsi bungeni akitaka hukumu ya kifo katika hatua ambayo sio tu kwamba ingefanya uhusino wa jinsia moja kati ya wanaume kuwa kosa la uhalifu lakini pia kuwahukumu kifo waliohusika na mahusiano hayo.

Lakini mataifa ya Magharibi yaliyopinga vikali hatua hiyo, huku Amerika, Uingereza na Canada zikiongoza, hayajawa yakitambua haki za LGBTQ kila wakati.

Mnamo Julai, kulikuwa na gwaride kubwa na la kifahari jijini London, kusherehekea miaka 50 ya mapambano, ya jamii ya LGBTQ ya Uingereza.

Wakati gwaride la kwanza lilipofanywa 1972, ilikadiriwa kuwa watu 2,000 waliowakilisha jamii hizi waliandamana, lakini mnamo Julai, makundi yaliyokadiriwa kuwa 600 ya aina tofauti za LGBTQ, wanasema waandalizi, yalipeleka watu 1.5 milioni katika barabara za London katika maandamano ya kwanza yaliyohudhuriwa na watu binafsi tangu kuzuka kwa Covid-19.



Rais wa Amerika Joe Biden

Meya Sadiq Khan alitaja Gwaride hilo kuwa sherehe ya jamii, umoja na ufanisi, lakini akaharakisha kuambia wanahabari kuwa kampeni hiyo haiwezi kuridhisha katika juhudi za kutaka kuwa na ulimwengu wazi, mjumuishi na unaokubali.

Alikuwa akifahamu ukweli kuwa wiki moja iliyotangulia, jijini Oslo, Norway, watu wawili walikuwa wameuawa na 20 kujeruhiwa katika shambulizi katika Gwaride la Kifahari.

Kwa nini gwaride za LGBTQ ni muhimu? Kwa sababu, linasema shirika la kutetea haki za binadamu la Amnesty International, watu bado wanashambuliwa kwa sababu ya chaguo lao la ngono na jinsia zao hata wakati wa kujionea fahari. Hafla hizi huwa fursa ya kupinga sheria za kuchukia mashoga na waliobadilisha jinsia na kuchangia mabadiliko ya moyo na akili.

Kwa hivyo, ni mambo gani yameafikiwa baada ya miaka 50 ya magwaride ya Fahari? Utafiti wa jarida la Stonewall Research wa mwezi Februari ulionyesha kuwa katika miaka ya sabini: "Habari za Mashoga, gazeti la kwanza Uingereza lilianzishwa. Switchboard, shirika la habari na kutoa usaidizi lenye makao London linalohudumu hadi wakati huu, lilianzishwa.

Kongamano la kwanza la watu waliobadilisha jinsia lilifanywa jijini Leeds na kongamano la kwanza la chama cha wafanyakazi mashoga na wasagaji lilifanywa kujadili haki zao wakiwa kazini. Katika tukio la kukumbukwa, "Maureen Colquhoun akawa mbunge wa kwanza wa Uingereza kukiri hadharani kuwa msagaji."

Baadaye miaka ya 2000, chini ya Waziri Mkuu Tony Blair, jarida la Stonewall lilisema sheria kadhaa zilianzishwa. "Serikali ya Uingereza iliondoa marufuku ya watu mashoga na wasagaji katika vikosi vya usalama. Pia tuliona Sheria ya Ushirikiano wa Jamii na Sheria ya Kutambua Jinsia zilianzishwa mwaka wa 2004 na kuwapa wanandoa wa jinsia moja haki sawa na watu walio katika ndoa.

Baadaye leo jarida hilo linasema: "tukitazama karibu nasi leo, ni wazi kuwa hatuna usawa... Ingawa tunajua hatua zimepigwa, bado tunapigana na mtazamo wa kurudi nyuma katika jamii.. ubaguzi kuhusu wanaume mashoga na walio na jinsia mbili wanatumiwa kuhalalisha ghasia na lawama kwa waaathiriwa wa mashambulizi. Mwaka wa 2022, bado hatuko salama katika jamii zetu."

Uingereza inapongezwa, kwa mfano, kwa kuwa na watu wengi Zaidi wa jamii ya LGBTQ katika bunge ulimwenguni ikiwa na jumla ya wabunge 62 wa jamii hiyo katika bunge la wanachama 650. Mbunge wa kwanza wa jamii hiyo alihudumu bungeni kati ya 1593 na1598. Waziri wa kwanza shoga aliteuliwa mnamo 1910 kuwa Waziri wa Koloni (nchi zilizotawaliwa na Uingereza wakati huo).

Tangu wakati huo, chama cha Labour kimetoa wanachama 12 wa LGBTQ mawaziri, chama cha Conservative kimetoa mawaziri wawili na mmoja kutoka chama cha Liberal na cha Liberals.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

UHUSIANO WA KARIBU KATI YA ALIYEKUWA WAZIRI MKUU NA BINTI YAKE

# NDIYE SIKIO LA MFALME?

*Mpangilio unaomuweka Winnie Odinga ndani ya shughuli zote za kisisisa za Raila umezua malalamishi mengi, sababu kuu ikiwa kwamba anawaharibia watu fulani walioweza kumfikia kwa urahisi na kumshawishi baba yake*

• NA OSCAR OBONYO

Alipoulizwa katika mahojiano na gazeti miaka mitano iliyopita kuhusu kazi anayofanya kujikimu maishani, Winnie Odinga alijibu, “Namhudumia baba yangu, mimi ni mlinzi wake.” Ingawa fupi, jibu hilo ni sahihi kwani linaonyesha jinsi kitinda mimba huyo wa aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga, alivyojipata katika mizozo ya baada ya uchaguzi na siasa za urithi katika familia ya Odinga.

Kwa muda mrefu ameibuka kuwa mshirika wa karibu zaidi na wa kuaminika, ambaye husitiri habari muhimu kuhusu kampeni na shughuli zingine za kisiasa za Bw Odinga.

Hata hivyo, ushawishi wake katika shughuli za kisiasa za baba yake umeibua malalamishi mengi kutoka kwa washirika wa mwanasiasa huyo mkongwe.

Hii ni kwa sababu amewazuia baadhi ya washirika wa Odinga kumfikia kwa urahisi, tofauti na ilivyokuwa zamani.

Mienendo yake iliwakera wengi wakati wa kampeni za uchaguzi wa Agosti 9. Alilaumiwa kwa kiburi, kutwaa biashara ya mabango ya kampeni, kuajiri na kufuta kiholela wafanyakazi katika ofisi ya kushirikisha kampeni za urais na kuzuia baadhi ya wanasiasa wakuu kumfikia Bw Odinga.

Malalamishi yamekuwa mengi kuhusu Winnie. Inasemekana wafanyabiashara wengi matajiri kutoka eneo la Mlima Kenya walikerwa zaidi na mienendo yake.

Magavana wawili wa ODM kutoka Nyanza na Magharibi mwa Kenya walilalamika kwa Odinga kuhusu mienendo ya binti yake. “Lakini wazazi wake ndio waliompa nafasi hiyo kwa hivyo hawangemkaripia. Badala yake walimpongeza kwa juhudi zake za kuhakikisha ushindi,” akasema mwanasiasa kutoka Pwani.

Mwanasiasa mwingine kutoka eneo la Mlima Kenya alilalamika kuhusu muziki wa reggae wakati wa kampeni, akisema ulitumiwa na viongozi wa kidini kumuonyesha Odinga kuwa mpinga Kristo. Lakini kwa kuwa anapenda reggae, anasema mwanasiasa huyo, Winnie na vijana wenzake walipuuza malalamishi yao.

Waliozungumza na Darubini ya Wiki kuhusu suala hili waliomba tusitaje majina yao. Sababu zinaweza kuwa mbili – kuwa Winnie ana uwezo mkubwa au hawataki kumkwaza Raila kwa kuonekana kumshambulia binti yake.

Juhudi zetu za wiki mbili za kutaka kupata kauli ya Winnie kuhusu lawama dhidi yake hazikufaulu kwani hakujibu simu zetu wala jumbe fupi tulizomtumia kwa simu yake ya mkononi. Lakini Seneta wa Siaya Dkt Oburu Oginga anamuondolea lawama mpwa wake. Anasema Winnie alikuwa mfanyakazi, sawa na wengine, akifanya kazi chini ya Bi Elizabeth Meyo, Afisa Mkuu Mtendaji (CEO) wa kituo cha kushirikisha kampeni za urais za Odinga.

Dkt Oginga anadai Winnie analaumiwa sababu anatoka familia ya Odinga, na ambaye, tofauti na wafanyakazi wengine, aliweza kumfikia mgombea urais. “Winnie alikuwa mfanyakazi mwaminifu aliyefanya kazi kwa kujitolea na kama ndugu yangu angeshinda, leo tungekuwa tunamsifia msichana huyu ambaye sasa tunamlaumu.”

Vitendo vya Winnie vimevutia pongezi na shutuma za Wakenya. Kwa mfano, hata kabla ya Mahakama ya Upeo kutoa uamuzi wake wa mwisho wa kesi ya Azimio ya kupinga ushindi wa William Ruto, Winnie alifuta ujumbe alioandika katika mtandao kuwataka wafuasi wa Odinga wajitokeze kwa maandamano.

Wakati huo pia kulikuwa na jumbe nyingi kutoka kwa akaunti yake ya Twitter akilumbana vikali na wafuasi na wapinzani wa Azimio. Baadaye alidai akaunti yake ilikuwa imedukuliwa. Kupitia jumbe za Twitter wikendi iliyopita, Winnie aliweka picha akitangamana na waumini baada ya ibada ya kanisa eneobunge la Kibra, hatua iliyoonekana kuashiria mipango yake ya kisiasa siku za usoni. Inasemekana pia ODM kinaweza kumteua kwa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), awakilishe vijana.



Winnie Odinga amekuwa mmoja wa wasiri wa baba yake. PICHA | MAKTABA

Je, hiyo ina maana anatayarishwa na familia ya Odinga kurithi mamlaka kutoka kwa Raila? Ama yeye ni msumbufu tu ambaye, bila kujua, huvuruga mipango ya kisiasa ya familia ya Odinga?

Wachanganuzi wanaamini Winnie anatekeleza wajibu wake wa kulinda masilahi ya baba yake. Kwa mtazamo wa Odinga, yeye ni msaidizi ambaye, kando na kushughulikia kazi za ofisi yake, husimamia pesa na akaunti za mitandao ya kijamii za kiongozi huyo wa ODM. Pamoja na majukumu ya kibinafsi ya kushughulikia afya ya baba yake, Winnie, 31, ndiye anayefaa zaidi kwa mahitaji ya Odinga.

Wajibu wake wa masuala ya ndani ya Odinga ulionekana Machi 9, 2018 alipoandamana na baba yake na Mbunge wa Suna Mashariki, Junet Mohamed, kukutana na Rais Uhuru Kenyatta katika jumba la Harambee House, mkutano uliozaa mwafaka wa kisiasa kati ya Odinga na Uhuru, maarufu kama “handisheki”.

Mtu wa familia ya Odinga anasema uhusiano wa karibu kati ya Odinga na kitinda mimba wake unatokana na uaminifu. Inasemekana Odinga amekuwa na shida kuhusu uaminifu kwa miaka mingi, baada ya kusalitiwa na marafiki wake wa karibu, washirika wa kisiasa na hata wasaidizi. Yeye na wengine walipoongoza kampeni za Ukombozi wa Pili kupitia maandamano barabarani miaka ya 1980 na 1990, inaaminika wenzake walichangia kukamatwa kwake mara kadha na maafisa wa usalama na kupelekea kufungwa jela kwa jumla ya miaka tisa.

Usaliti huo, tunaarifiwa, uliendelea hadi 2017, ambapo watu ambao Odinga aliwaamini kusimamia pesa za kampeni,

Endelea Uk 11

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ ENEO LAKATA TAMAA KWA MRADI KENYA

# NYANZA KATIKA NJIAPANDA

*Ni nani atarithi Raila iwapo ataamua kustaafu siasa? Hakuonekani kuwa na mwanasiasa hata mmoja aliye na haiba na ujasiri mwenye nguvu na uwezo wa kifedha kama kiongozi huyo wa Azimio*

● Na JOSEPH MBOYA

Ushindi wa Dkt William Ruto dhidi ya Raila Odinga katika uchaguzi wa urais wa Agosti 9 ulikuwa na athari kubwa kwa siasa za jamii ya Luo.

Huku uzee ukimuandama, wengi hawafikirii Raila atagombea urais 2027. Maswali yanaulizwa iwapo kiongozi huyo wa Orange Democratic Movement (ODM) atakuwa na umaarufu ambao amekuwa nao katika jamii ya Waluo tangu miaka ya tisini. Alirithi kura za eneo hilo kutoka kwa baba yake, aliyekuwa Makamu Rais wa kwanza wa Kenya, Jaramogi Oginga Odinga.

Umaarufu wa Jaramogi katika siasa za jamii ya Waluo ulikuwa mkubwa hivi kwamba, wakati mmoja, Waziri Stanley Oloitiptip alisema kwa Waluo "Gor Mahia (klabu ya soka) ni dini na Oginga Odinga ni mungu wao".

Hadi kuuawa kwa Tom Mboya mnamo Julai 5, 1969, Waluo wakiwa wamevunjika moyo na kukata tamaa na serikali ya Kenya, Jaramogi alichukua hatua haraka akatumia wimbi la maombolezo kuvuta Waluo upande wake. Aliibuka kuwa kiongozi wa Waluo na jamii hiyo ikawa ya watu wanaozungumza kwa sauti moja katika masuala ya kitaifa.

Wakati pekee ambao Jaramogi alienda kinyume na matakwa ya watu wake ilikuwa wakati wa mzozo uliogonga vichwa vya habari kuhusu alikofaa kuzikwa wakili mashuhuri wa kesi za uhalifu SM Otieno. Ingawa mjane wake, Wambui Otieno, alitaka wakili huyo azikwe eneo la Upper Matasia, Ngong, ukoo wake wa Umira Kager ulitaka Otieno azikwe Nyalgunga, Kaunti ya Siaya.

Umira Kager, kupitia wakili wao, Richard Otieno Kwach, walishikilia kuwa Waluo wanafaa kuzikwa katika ardhi ya mababu zao. Wambui alipinga akisema Otieno alitaka azikwe Ngong. Shida iliyokuwepo ni kuwa wakili huyo hakuwa ameandika wosia kabla ya kifo chake.

Kesi ilipokuwa ikiendelea kortini, Jaramogi alisema hadharani kuwa walipounda Muungano wa Waluo, ilikubaliwa kuwa Waluo wanaweza kuishi popote na kuzikwa huko. Kwach alikasirika na kumtaja Jaramogi kuwa "mwanasiasa mzee aliyeisha."

Katika uchaguzi wa Agosti, Raila aliagiza Waluo wachague wagombeaji wa Azimio pekee. Agizo hilo lilifuatwa kikamilifu isipokuwa David Ochieng wa Ugenya aliyechaguliwa mbunge kwa chama cha MDG.

Huku Rais William Ruto akishikilia usukani, inaoenekana kwa mara nyingine Waluo wamerudi pale pale walipozoea - katika upinzani. Wafuasi wa Raila, hata hivyo, wanaamini alipokonywa "ushindi". Jamii hiyo inahisi imetengwa kutoka Kenya. Baadhi ya watu wa jamii hiyo wanatoa mapendekezo kuhusu jinsi ya kuunda eneo la Waluo bila kuwa sehemu ya serikali.

Kuna vuguvugu linalotaja Waluo kuwa Igbo wa Kenya. Mnamo 1967, Luteni Kanali Chukuwumeka Ojukwu alitwaa silaha kupigania kuundwa kwa Jamhuri ya Biafra (Igbos) kutoka kwa serikali ya majimbo ya Nigeria iliyokuwa ikiongozwa na Jenerali Yakubu Gowon. Vilikuwa vita vibaya ambapo watu wengi walikufa.

Waliotaka kujitenga waliposhindwa, jamii ya Igbo iliweka moyo wake katika mwelekeo mpya - elimu, biashara na sanaa. Tangu wakati huo wametawala sekta hizo ikiwemo ya sinema ya Nigeria ambayo kwa wakati huu inakadiriwa kuwa ya pili ulimwenguni kwa idadi ya sinema.

Wanaounga hatua ya kujitenga wanaamini eneo la Luo Nyanza lina rasilimali nyingi, ambazo zikisimamiwa vyema, zinaweza kulifanya kustawi kiuchumi. Ni kweli. Ziwa Victoria lina uwezo mkubwa ambao haujawahi kutumiwa. Hatua ya kwanza inaweza kuwa uwekezaji mkubwa katika sekta ya uvuvi kusaidia wavuvi katika ziwa hilo kupata mashua za kisasa na vifaa vingine vya uvuvi.

Hii inafaa kufuatiwa na uwekezaji katika vifaa baridi na vituo vingine vya kuhifadhia samaki vyema na pia viwanda vya kutayarisha samaki.



Thomas Joseph Odhiambo 'Tom' Mboya ni kiongozi aliyeheshimiwa katika jamii ya Waluo. Alifariki Julai 5, 1969.

Kuna soko kubwa kwani kwa sasa samaki wanatoka China. Watu wanaojua vyema ulaji wa samaki watakwambia tofauti kati ya ubora na ladha ya samaki kutoka Ziwa Victoria na wanaotoka China ni sawa na Mashariki na Magharibi.

Utalii unakaribiana na Uvuvi. Kisumu Impala Sanctuary inapatia wageni nafasi ya kutazama swara, chui, nyati na simba miongoni mwa wanyama wengine. Kit Mikayi, mwamba wa ajabu ni kivutio kikuu. Kisha unaweza kuvuka ziwa ndani ya feri au meli hadi kisiwa cha Rusinga. Karibu na kisiwa hicho kuna Mbuga ya Kitaifa ya Ruma. Wanaotaka kutembelea makavazi ya kaburi la Tom Mboya pia wanaweza kushirikishwa katika safari hiyo.

Suala kuu linalofuata linahusu atakayemrithi Raila akiamua kustaafu kutoka siasa. Hakuna mwanasiasa hata mmoja aliye na ushawishi, ujasiri na pesa kama kiongozi huyo wa Azimio.

Magavana Anyang' Nyong'o na James Orengo wametajwa kuwa wanaoweza kumrithi Raila. Lakini umri wao ni sawa au chini kidogo na wa Raila. Aliyekuwa Gavana wa Nairobi, Evans Kidero, pia ametajwa. Ana pesa na umri wake ni mdogo. Baraza la mawaziri la Ruto lina mtu pekee kutoka jamii ya Waluo, Eliud Owalo. Kuwa waziri wa pekee (iwapo bunge litamuidhinisha) kutoka eneo hilo kunampa Owalo nafasi nzuri ya kujijenga kisiasa.

Hata hivyo, waliowahi kufanya kazi naye wanaamini kuwa Owalo ni mtaalamu zaidi kuliko mwanasiasa na hawezi siasa za kijamii. Kuna wale wanaodai kuwa Owalo hatangamani na watu eneo hilo. Lakini kwa jumla, kuna hisia za kukata tamaa miongoni mwa Waluo na Mradi Kenya.

Kwa sababu ya mwelekeo wa kisiasa, eneo hilo limekuwa katika upinzani tangu 1966. Kumekuwa na minong'ono kwamba kuwa na jina la Mluo Kenya ni mzigo hasa kwa wanaotaka kufanya kazi katika utumishi wa umma.

Hii pengine ndiyo sababu kuna mtindo mpya wa kuwapa watoto majina katika jamii hiyo. Badala ya majina kama Otieno, Akinyi na Odhiambo, wazazi wengi sasa wanatumia majina kama Hera (love), Gweth (baraka) na Hawi (bahati). Hata hivyo, wanaochagua majina kama hayo wanatajwa kuwa Waluo matajiri na watu wa jamii hiyo walio na misimamo mikali.

*osephmboyaa@gmail.*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

RUTO ALENGA KUKUZA MASOKO YA MTAJI

# SHIDA KATIKA UBINAFSISHAJI

*Kukiwa na tume ya ubinafsishaji ambayo imekaribia kufa, maamuzi muhimu kuhusu uunganishaji, makubaliano, shughuli za pamoja na uuzaji wa mali ya serikali yanafanywa na taasisi zingine za serikali*



Rais William Ruto wakati wa sherehe ya kupiga kuzindua upya Soko la Hisa la Nairobi (NSE), eneo la Westlands, mnamo Jumanne. Karibu naye ni Naibu Rais Rigathi Gachagua (kushoto) na mwenyekiti wa NSE Kiprono Kittony. PICHA I PSCU

NA JAINDI KISERO

Kwa Rais William Ruto, sherehe ya kupiga kengele aliyoongoza katika Soko la Hisa la Nairobi mnamo Jumanne, ilikuwa fursa ya kufufua ahadi ya serikali mpya ya kutia nguvu mpya mipango yake ya kukuza soko la mtaji, kwa kuidhinisha hisa zaidi za mashirika ya kibiashara ya serikali chini ya mpango wa ubinafsishaji.

Lakini kilichosisimua katika hafla hiyo ni tukio la ucheshi Rais alipokemea maafisa wawili wa umma waliokuwa katika hafla hiyo kwa utendakazi duni na kupata mishahara minono bila kufanya kazi. "Mnafaa kurudisha pesa ambazo tumetumia kuwalipa mishahara," akasema. Wanaume hao wawili waliomulikwa ni Afisa Mkuu Mtendaji wa Tume ya Ubinafsishaji (PC), Bw John Kosgey na Mkurugenzi wa shirika la kifedha la Nairobi International Financial Centre (NIFC), Bw Oscar Njuguna.

Rais alisema PC haikuwa imetayarisha shughuli yoyote kwa miaka 13 iliyopita. Alisikitika kuwa NIFC, licha ya kubuniwa miaka mitano iliyopita, ilikuwa imesajili mwekezaji mmoja pekee.

Je, rais alikuwa akiashiria mabadiliko makubwa katika mashirika hayo? Inangojewa kuonekana. Vituko vikubwa vya siri na vya hivi punde katika ubinfsishaji vinahusu hoteli mbili maarufu Nairobi - Intercontinental na Hilton.

Kampuni hizi mbili muhimu ulimwenguni zimeondoa uwekezaji wake katika hoteli hizi mbili za kifahari ambazo zimekuwa zikihudumu tangu 1969.

InterContinental Group na washirika wake hapa nchini - shirika la kiserikali la Tourism Finance Corporation (TFC), na kampuni inayomilikiwa na familia ya Moi - Sovereign Trust Limited na benki inayomilikiwa na serikali ya Development Bank of Kenya (DBK) - hivi majuzi zilitangaza kuuza hoteli hiyo, na kualika mapendekezo kutoka kwa kampuni za uuzaji mali kukodisha au kubadilisha jengo hilo kwa matumizi tofauti.

Athari za kujiondoa kwake ikiwemo kupoteza ajira, nafasi ya nchi kama kituo cha utalii na sifa zake kama kituo bora cha uwekezaji zitakuwa kubwa.

Kwa nini ikawa hivyo? Ukifuatilia rekodi za tangu mkutano wa baraza la mawaziri mnamo 2009, ambapo iliamuliwa hisa za serikali katika hoteli tatu zilizomilikiwa na TFC - ambazo ni Hilton, InterContinental na Mountain Lodge - zibinafsishwe, utapata kuwa Wizara za Utalii, Fedha na Tume ya Ubinafsishaji (PC) hazikufanya maamuzi yanayofaa.

Ushahidi kutokana na rekodi hizo unaoneysha kuwa watu wenye ushawishi hapa nchini wanafanya mambo kisiri; kwanza, kuzima juhudi za wawekezaji wa kigeni za kuweka pesa katika biashara hizo; pili, kufanya thamani ya mali hiyo kupungua, na mwisho, kuwezesha washirika wa walio mamlakani kunyakua ardhi na majengo hayo kwa bei ya chini.

Inaonekana mpango huo ulitekelezwa kwa awamu mbili, Kwanza, wawekezaji wa kigeni walizuiwa kabisa kuweka mtaji katika biashara hizo na kuambiwa wasubiri hadi baada ya serikali kujiondoa katika kampuni hizo. Katika awamu ya pili, kulikuwa na vituko vingi vya siri vilivyohakikisha ubinafsishaji haukufanyika ilivyopangwa.

Mnamo Julai 2014, aliyekuwa Afisa Mkuu Mtendaji wa TFC, Marianne Ndegwa Jordan, alimwandikia barua Waziri wa Fedha, Henry Rotich, akiomba serikali ikubali ubinafsishaji uendelee. Alimfahamisha waziri kuwa wawekezaji kutoka Amerika walikuwa tayari kuweka dola 75 milioni kukarabati hoteli hiyo na walikuwa wamechoka kusubiri ubinafsishaji uliopangwa.

Wawekezaji wa kigeni walipokuwa wakiambiwa wangoje, thamani ya hoteli hiyo iliendelea kushuka. Mbinu na ujanja za kampuni ya Sovereign Trust inayomilikiwa na familia ya Moi zilichangia katika kuahirishwa kwa ubinafsishaji huo.

Mawasiliano yanaonyesha kuwa ubinafsishaji ulipokuwa karibu kuanza mapema 2014, familia ya Moi iliandikia Tume ya Ubinafsishaji, ikitaka kununua hisa zilizomilikiwa na serikali katika hoteli hiyo kwa Sh1.9 bilioni (Sh325 kwa kila hisa).

Miezi michache baadaye, makarani wa kampuni ya InterContinental Group walipokea barua nyingine ambayo familia ya Moi ilipunguza pesa ilizotaka kulipa hadi Sh628 milioni (Sh107 kwa hisa) ambazo Tume ya Ubinafsishaji ilikataa. Ubinafsishaji uliporomoka.

Baraza la Mawaziri lilikuwa limeagiza hisa hizo zibinafsishwe kwa kuruhusu wenyehisa wa hapa nchini kuzinunua kwanza. Hivyo basi, Sovereign Trust, ikiwa na asilimia 19.38 ya hisa, ilikuwa katika nafasi nzuri ya kuzinunua. Wenyehisa waliobaki wa humu nchini wana hisa chache. Hisa zingine nyingi katika kampuni hiyo ni asilimia 10 zinazomilikiwa na TransCentury Group kupitia DBK, ambayo ina asilimia 12.99 katika hoteli hiyo.

Makamishna wote waliopin-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya



Mkuu wa NIFC Oscar Njuguna

ga hatua ya kijanja ya kampuni ya Sovereign Group walimaliza mihula yao na kuondoka. Afisa Mkuu Mtendaji, Bw Solomon Kitungu, pia aliondoka na nafasi yake ikachukuliwa na Afisa Mkuu Mtendaji wa sasa, Bw Joseph Koskey, ambaye alikuwa Afisa Mkuu Mtendaji wa Sovereign Group.

Yaliyofanyika katika Hilton Group si tofauti. Wamiliki wake, raia wa Amerika, wamezuiwa kukarabati hoteli hiyo huku serikali ikijikokota katika mipango yake ya kuuza hisa zake asilimia 40.5 zinazomilikiwa na TFC kwa niaba yake katika hoteli hiyo.

Tume ya ubinafsishaji ikiwa imekaribia kufa, maamuzi muhimu kuhusu kuunganishwa kwa mashirika, makubaliano, shughuli za pamoja na uuzaji wa mali ya serikali yanafanywa na taasisi zingine za serikali.

PC ilitekeleza wajibu mdogo katika uuzaji wa National Bank of Kenya kwa Kenya Commercial Bank. Haikuhusishwa katika jaribio lililotibuka la serikali mwaka wa 2018 la kuunganisha Kenya Airways na Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Jomo Kenyatta na kubuniwa, kupitia agizo kuu la rais, kwa shirika linalofahamika kama Kenya Transport and Logistics Network la kushirikisha shughuli za Mamlaka ya Bandari Kenya, Shirika la Reli la Kenya na Kampuni ya Mafuta ya Kenya.

Mwaka jana, Waziri wa Utalii, Najib Balala, alitangaza kuwa TFC ilikuwa imevunjwa na kuwa shughuli zake zitaunganishwa na zile za ICDC na IDB Capital kuunda shirika jipya la Kenya Development Bank Corporation.

Mkanganyiko huu na ukosefu wa uwazi katika shughuli hizi ulizidishwa na ukweli kuwa PC haikuwa na bodi kwa muda mrefu, na hali hiyo ilifanya tume hii muhimu kushindwa kutimiza majukumu yake.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

# Hapa ndipo NIFC ilifeli

• NA JAINDI KISERO

Malalamishi ya Rais William Ruto kuhusu utendakazi wa shirika lililosifiwa sana la Nairobi International Financial Centre, alipohudhuria hafla katika Soko la Hisa la Nairobi, yamemulika mmojawapo wa miradi iliyosifiwa sana nchini.

Akizungumza na Afisa Mkuu wa kituo hicho, Bw Oscar Njuguna, Rais alisema Wakenya watataka arudishe pesa zilizotumika kumlipa mshahara. Bw Njuguna alikuwa afisa mkuu wa kituo maarufu ulimwenguni cha Qatar International Financial Centre.

Kenya imekuwa ikipanga kuanzisha kituo cha kimataifa cha fedha kama hicho tangu Bunge lilipopitisha Sheria ya NIFC mnamo 2007. Huenda tatizo kuu limekuwa muundo ambao Kenya imetumia.

Serikali iliacha mbinu bora za kimataifa, ambapo vituo vya kimataifa vya fedha vinaundwa kwa mpango wa maeneo ambayo yako na watoaji huduma za kifedha kama benki za kibiashara, benki za uwekezaji, na hazina za uwekezaji na masoko ya hisa.

Nchi nyingi huanzisha miradi ya ujenzi wa maeneo spesheli kuwa ya kifedha. Nchi jirani ya Rwanda ilikumbatia mbinu hiyo ya kujenga maeneo spesheli ya kifedha. Mwaka jana, ilitangaza kuwa ilipatia Benki ya Equity kandarasi ya kujenga jumba la Kigali Financial Towers ambamo kutakuwa na Kigali International Financial Centre.

Kenya imeanza kituo cha fedha bila eneo spesheli. Kusema kweli, serikali imesema wazi kuwa mwekezaji yeyoteataruhusiwa kokote nchini mradi tu awe na cheti kutoka kwa Mamlaka ya NIFC.

Tajiriba ya kimataifa imeonyesha kuwa wawekezaji huvutiwa na vituo vya kifedha nchi ikiwa na yafuatayo: Kwanza, shirika huru la serikali kutangaza, kuunda na kusimamia kituo hicho, mamlaka ya kutoa leseni iliyo na sajili ya kampuni ya kushughulikia wanaotaka leseni katika kituo hicho.

Rwanda imeunda shirika spesheli linaloitwa Rwanda Finance kutangaza Kigali International Financial Centre.

Pili, shirika huru la usimamizi na udhibiti, linalohudumu kama sekta spesheli ya kudhibiti sekta ya fedha kwa eneo hili maalumu la uchumi.

Nchini Dubai, Gavana wa benki kuu ndiye pia mwenyekiti wa Dubai International Financial Centre.

Mwisho, mahakama ya upatanishi iliyoundwa spesheli kuhudumia wanaopewa leseni za kituo cha kimataifa cha fedha na iliyo na uwezo wa kutatua mizozo na kandarasi kwa kuzingatia sheria za kimataifa.

Badala ya kuunda shirika huru la usimamizi, Kenya ina kamati ya uelekezi iliyojaa washirika wa wanasiasa, wakiwemo rais na naibu wake.

Badala ya mahakama ya upatanishi na mazingira bora ya kisheria kwa kutumia muundo wa mfumo wa Jiji la London, tunapendekeza jopo dogo kwa mujibu wa sheria za Kenya.

Wazo hilo lilipobuniwa kwa mara ya kwanza, Kenya ilitaka kujenga eneo la kifedha linalofanana na maeneo spesheli ya kiuchumi kutoa huduma za kifedha za kimataifa na kuwa na taasisi za kimataifa na za humu nchini zilizochaguliwa.

Lengo lilikuwa kuunda sekta kubwa ya uchumi wa jiji, jiji ndani ya jiji kwa muundo wa vituo vya kimataifa vya fedha kama vya Mauritius, Hong Kong au Singapore.

Kuna wakati Wizara ya Fedha ilizungumza na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (KAA) kutoa ardhi ambako eneo hilo lingejengwa.

Iwapo mbinu ya Kenya itafaulu, inangojewa kuonekana. Tajiriba ni kuwa sheria na afueni ya ushuru pekee hazifanyi vituo vya kimataifa vya fedha kufaulu.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

# Winnie ndiye Mteule?

Kutoka Uk 8

yakiwemo malipo ya maajenti wa kura, wanadaiwa kutoweka na pesa hizo. Inadaiwa baadhi yao walinunua majumba ya kifahari jijini la Nairobi.

Na kama kuthibitisha hofu yake, msichana aliyekuwa msaidizi wa mkewe Odinga, Mama Ida, alitoweka baada ya uchaguzi mkuu wa Agosti 9 na baadaye akatangaza kumuunga mkono Rais William Ruto. Msichana huyo, maarufu ndani ya Azimio/ODM kama "Terry Chocolat" au Terry, aliaminika kuwa miongoni mwa majasusi wa kambi pinzani aliyefaulu kupenya katika kampeni za Odinga.

"Huyu ndiye msichana aliyepangia viti kwa nyumba na kutupatia maji au jusi wakati wa kampeni tulipomtembelea Baba nyumbani kwake Karen au makao yake katika Shamba la Opoda," anasema mmoja wa magavana wa ODM.

Terry, ambaye anatoka Siaya, baadaye alidai alihama kambi ya Odinga kwa sababu ya "kiburi cha binti yake" na madai ya Winnie kuwadhuluma washirika wengi wa kampeni za Odinga. Licha ya yote hayo, ni tangazo lake kuhusu mapenzi yake kwa familia ya Ruto lililozindua kundi la kampeni la Odinga.


Kutokana na tukio hili na mengine ya awali, uamuzi wa kumteua binti yake kuwa msaidizi na msiri wake unaeleweka. Inasemekana siku za hivi majuzi Odinga amekuwa na tahadhari kubwa katika shughuli zake, na haya yanaelezea ni kwa nini anaamini watu wachache. Mmoja wao ni Mohamed, mkurugenzi wa uchaguzi wa ODM, Katibu Mkuu wa Azimio - One Kenya na Kiranja wa Wachache katika Bunge la Kitaifa.

Kando na kumsaidia katika siasa, Winnie anaonekana kuwa mrithi wa kiti cha enzi cha baba yake – kwa hali na mpango.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# habari kwa picha




Richarlison wa Tottenham Hotspur (juu) amruka Evan N'Dicka wa Frankfurt wakati wa mechi ya Ligi ya Mabingwa Kundi D jijini London mnamo Oktoba 12. Spurs walishinda kwa 3-2. PICHA I AFP




Maafisa wa Kitengo cha Kupambana na Majanga (DRU) cha Jeshi la Kenya (KDF) wakiondoa vifusi katika eneo ambako jumba linalosemekana lilijengwa kwa vifaa duni liliporomoka eneo la Kirigiti, Kaunti ya Kiambu, mnamo Septemba 26. PICHA I AFP



Mwanamume amsaidia mwanamke aliyejeruhiwa wakati wa maandamano ya kumtaka Waziri Mkuu wa Haiti, Ariel Henry, ajiuzulu, jijini Port-au-Prince, mnamo Oktoba 10. PICHA I AFP





Ruth Chepngetich wa Kenya akisherehekea baada ya kumaliza mbio za Chicago Marathon mnamo Oktoba 9. PICHA I AFP



Mwanasarakasi awasili katika siku ya mwisho ya mashindano ya sarakasi ya New York Comic Con 2022, katika eneo la Jacob Javits Center, jijini New York, mnamo Oktoba 9. PICHA I AFP



Wanajeshi wa Jeshi la Korea Kusini wa kikosi cha mstari wa mbele cha makombora ya masafa marefu na kile cha angani wakati wa mazoezi ya mashambulizi katika eneo lisilojulikana mnamo Oktoba 6. PICHA I AFP



Mapango ya Kome katika jimbo la Berea, nchini Lesotho, mnamo Oktoba 9. Vyumba hivyo vya udongo, vinavyotumiwa kama Makavazi ya Kitaifa, awali vilikuwa maficho ya watu wa koo za Basia na Bataung wakati wa Vita vya Lifaqane (Vita vya Mfecane) na ulaji wa nyama za watu katika karne ya 18. PICHA I AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"



# MITINDO

*Baada ya kuwavisha wasanii watajika, wanasiasa maarufu na wanahabari, Mawia Muthengi anaelekeza mtindo wa Kiafrika katika kiwango kipya*

NAFASI YA VIJANA

# MKAKATI KAMILI AMBAO ULIFAULU

**HASLA:** Ujumbe wa kampeni uliundwa ili kujumuisha kila mtu aliyekuwa na hofu kuhusu hali ya uchumi

• NA BILL KEMBO

Mpende, mchukie au mpuuze, Rais William Ruto aliwapiga wapinzani wake panna. "Panna" ni aina ya chenga katika mchezo wa kandanda ambapo mpinzani hupitisha mpira katikati ya miguu yako ukimkabili na kukuacha umeduwaa.

Siasa nchini zimekuwa, na zitaendelea kuwa, mchezo unaohusu kuleta pamoja watu kwa misingi ya kikabila. Makabila hayo yanaweza kuletwa pamoja na itikadi, sera au imani fulani, au haya yote.

Rais Ruto na wenzake katika muungano wa Kenya Kwanza, walifaulu kuunda kabila jipya. Kabila hilo liliitwa hasla, lenye alama ya wilibaro. Mbona suala hili lilileta mwamko mpya katika siasa za Kenya?

Ted Brader, katika kitabu chake, "Campaigning for Hearts and Mind – How emotional Appeals in Political Ads Work" anasema kauli mbiu za kisiasa hulenga kuamsha hisia kuhusu mambo mazuri yaliyofichika. Anatoa mfano wa kampeni ya aliyekuwa Rais wa Amerika, Ronald Reagan alipogombea urais muhula wa pili. Alitumia kauli mbiu "It's morning again in Amerika" (kumekucha tena Amerika). Kauli mbiu hii ilitungwa kwa lengo la kuibua hisia, mwamko na matumaini mapya. Chini ya utawala wa Reagan, uchumi wa Amerika ulionyesha dalili za kuimarika na wananchi waliingiwa na matumaini ya maisha mazuri.

Linganisha hii na kauli mbiu ya muungano wa Kenya Kwanza, "freedom is coming" (uhuru unakuja). Kauli hii ilionyesha serikali ya Uhuru Kenyatta, ambayo Raila Odinga alikuwa mshirika, kuwa dhalimu – kuwaandama raia, uchumi kuharibika, na hata vibaya zaidi, ilionyesha serikali isiyojali masilahi ya wananchi wa kawaida. Mpango ulikuwa gani? Kumhusisha Raila na hali hii kwa misingi ya ushirika wake na Uhuru kupitia handisheki. Tofauti na ilivyokuwa kwa Reagan, mambo hayakuwa mazuri nchini Kenya na hii iliibua hasira miongoni mwa wananchi.

Buni kabila la watu fulani, kisha wahamasishe kupiga kura kwa namna fulani kupitia kauli mbiu iliyoundwa kwa ustadi wa kipekee. Hii ilionekana kama mbinu iliyotumiwa na muungano wa Kenya Kwanza. Huwa ni rahisi kuchochea hisia za binadamu.

Woga ndio huchochea zaidi hisia za mwanadamu. Machafuko ya kisiasa yaliyotokea mnamo 2007 yalichochewa na woga ambao tuliwekewa kama makabila. Baadhi ya masuala yaliyotutia woga yalikuwa ya kweli au ya kudhaniwa tu, kabla na hata baada ya uchaguzi huo.

Tume iliyochunguza chanzo cha machafuko baada ya uchaguzi ilitaja malalamishi kuhusu umiliki wa ardhi na ukiritimba wa mamlaka katika asasi ya urais kama mambo makuu yaliyochochea ghasia hizo za kisiasa.

Kando na kutumia propaganda kwa ustadi, Kenya Kwanza pia ilifaulu kuwaelekeza wafuasi wake, na Wakenya kwa jumla, kwa suala la hali ya uchumi. Wito wa kuimarisha maisha ya mahasla ulisukwa ili kuwakilisha kila mtu, matajiri kwa masikini.

Katika manifesto yake, Kenya Kwanza iliahidi kuondoa shida hizi. Matokeo? Ujumbe huu ulipokewa vizuri miongoni mwa Wakenya. Uchumi uligeuka kuwa suala kuu kuelekea uchaguzi huo.

Muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya ulijipata ukijibu masuala ambayo yaliibuliwa na Kenya Kwanza. Hawakuona dalili kuwa wangeshindwa. Ahadi zake kama vile ruzuku ya Sh6,000 kila mwezi kwa familia maskini haikufua dafu kwa ile ya Ruto ya kuanzishwa kwa Hazina ya Mahasla ya Sh50 bilioni, ahadi ya kupunguza ushuru, manifesto bora, kampeni zilizopangwa vizuri na mkakati bora wa mawasiliano.

*Bw Kembo ni Mwanafunzi wa Taaluma ya Mawasiliano, Sera ya Umma na Sheria katika Chuo Kikuu cha London. Aidha, yeye ni mtaalamu wa Teknolojia ya Habari (IT).*

*Je, wewe ni mtu wa umri mdogo na una ndoto maishani? Tungetaka kusikiza kutoka kwako. Tuma maoni na/au kauli zako kuhusu mada mbalimbali kwa:*

***weeklyreview@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

## WANAVYOSEMA



**Caroline Mochoge**

Gharama ya juu inachangiwa kwa namna fulani na ufisadi. Bei za juu za chakula na mafuta zimefanya hali hii kuwa mbaya zaidi. Rais William Ruto anafaa kutimiza ahadi yake ya kusaidia wakulima na wafanyabiashara wadogo. Anahitaji kuhakikisha usimamizi mzuri wa pesa na kuepuka mtindo wa kukopa ili kufadhili shughuli za serikali. Aidha, anafaa kuunda mfumo mzuri wa ulipaji kodi wenye makataa thabiti.

*— Mtaalamu wa Mawasiliano*



**Hosea Otieno**

Wakenya wengi wanahangaika kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa za kimsingi. Serikali inafaa kupunguza ushuru wa VAT kwa bidhaa za kimsingi, kuhimiza uagizaji wa vyakula kwa kupunguza ushuru unaotozwa bidhaa kutoka nje na kupunguza pesa za miradi mikubwa. Serikali pia inafaa kuweka sera za kusaidia kilimo cha bidhaa za mafuta ya kupikia kama vile alizeti na ufuta. Huo ndio mwelekeo utakaookoa taifa letu.

*— Mwanafunzi wa Sheria, Chuo Kikuu cha Nairobi.*



**Walter Nalwa**

Serikali inafaa kughulikia ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana. Inafaa pia kutekeleza sera kuhusu mafunzi ya kiufundi na sekta ya "Jua Kali" ambayo inaweza kuchochea ukuaji wa uchumi na hivyo kupunguza gharama ya maisha. Suala lingine muhimu na kuimarisha uzalishaji katika sekta ya kilimo ili kumaliza mtindo wa kutegemea chakula kutoka nje.

*— Mwanafunzi, Chuo Kikuu cha Daystar*



**Samuel Mue**

Tunafaa kusaidia familia na jamii maskini ambazo zinakumbwa na changamoto mbalimbali. Hili halifai kufanywa kupitia chakula cha msaada bali kwa kupunguza ushuru ili kuimarisha uwezo wa familia maskini kujimudu. Tunafaa pia kuwasaidia wafanyabiashara wa hapa nchni na viwanda vidogo. Manufaa ya kufanya hivi yatafaidi Wakenya wengi.

*— Afisa Mkuu wa Kenya Model UN*

*- Zimetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MTAZAMO WANGU

# GMO: HATUA YA RAIS INASTAHILI



● NA WAGA ODONGO

**JAMBO LA KUZINGATIA:** Marufuku hiyo haikuwa na maana yoyote. Mbona ni lazima mazao yaliyosambazwa na kuliwa kwa njia salama katika maeneo mengine yafanyiwe



Kenya hivi majuzi iliondoa marufuku ya vyakula vilivyokuzwa kwa njia ya kisayansi (GM) na kutamatisha mwongo mmoja wa moja kati ya maamuzi mabaya zaidi kuhusu sera ya kilimo ambayo serikali imewahi kufanya.

Mkanganyiko uliopo kuhusu suala hilo unashangaza: Kenya ilikuwa miongoni mwa mataifa makuu katika utafiti wa nyanja hiyo, ilhali wanasayansi wetu walijikita tu katika majaribio nyanjani.

Nakumbuka nikikutana na wasomi watatu wa Uzamifu kutoka Ghana na Tanzania katika chuo kikuu cha umma wakisomea kozi ya bayotekinolojia katika taifa linalopinga taaluma hiyo. Serikali ilikuwa inafadhili raia wa kigeni kuja kutafiti mimea ya GM huku ikipuuza tafiti hizo hizo zinazofanya vyuo vyetu vikuu vya umma kuwa maarufu.

Marufuku hiyo haikuwa na maana yoyote. Kwa nini ni lazima mimea iliyotumwa na kuliwa kwa njia salama katika maeneo mengine ifanyiwe majaribio hapa nchini? Kuna mtu aliyefikiri kuwa mashirika yetu ya mimea yamefadhiliwa vyema zaidi au ni bora zaidi katika utafiti kushinda yale ya Amerika? Hiyo ni sera potovu iliyotokana na woga.

Lakini sasa tuna shinikizo la ziada kuhusu mimea ya GM. Baa la njaa linatafuna ardhi kwa mara nyingine tena. Rais mwingine tena anazindua rasmi usambazaji wa chakula cha msaada. Tuna idadi ya watu inayoongezeka kwa kasi, thuluthi mbili za nchi yetu ni jangwa, sayari yetu viwango vya joto vinazidi kuongezeka na tunahitaji chakula cha kutosha.

Wakati huo huo, bara la Afrika Mashariki limo katikati ya kipindi cha kiangazi kilichokithiri kwa miaka minne. Hali inaharibiwa zaidi na mazao yanayoendelea kudidimia. Uzalishaji wetu kwa kila ekari ya ardhi ni chini ya thuluthi moja ya jumla duniani. Ili kuweza kujilisha, tutalazimika kutenga ardhi zaidi kwa kilimo na wakulima wataangamiza ndovu wote hata kabla ya wawindaji haramu kufanya hivyo.

Tumaini letu bora, litakalokuwa la upesi na bila gharama kubwa ni kuanza kilimo cha mimea inayokuzwa kisayansi. Ni uamuzi ambao umechelewa kwa miongo mitatu.

Ushahidi unaounga mkono uamuzi huo ni chungu nzima: Mazao ya GM ni mazuri kwa wakulima na wanunuzi bidhaa. Kwa sababu ya hofu inayotokana na mimea hiyo, nafaka za GM hufanyiwa majaribio zaidi kushinda aina zinazopatikana nyikani zilivyowahi kufanyiwa. Aidha, tulipitisha hoja kuu kitambo. Vyakula hivyo vimeliwa kwa wingi kote duniani pasipo tatizo lolote.

Ekari nusu bilioni za ardhi ulimwenguni kote zinakuzwa GM. Mbali na tafiti tulizo nazo za kisayansi za kutupa mwongozo, tuna tafiti za tafiti kuhusu mimea ya GM na hakuna kasoro ilitotajwa. Kila hifadhi ya maarifa ya kisayansi yaliyokamilishwa inahitimisha kuwa GM ni salama kuliwa na binadamu.

Lakini bado kuna pingamizi tele. Hoja mojawapo ambayo imetolewa na wanaopinga ni kufuata mtazamo wa Uropa kuhusu vyakula vya GM. Haina mashiko. Wanaharakati wa Uropa wanaongozwa na wasiwasi wa dhana wala si utafiti wa kisayansi. Uropa haina jangwa na idadi ya watu wake inashuka kwa kasi.

Wana maziwa ya siagi na milima ya ngano. Serikali inayowalipa wakulima kuacha mashamba yao bila kupandwa chochote haiwezi utumika kama mfano wa kuigwa katika mataifa mengine.

Barani Afrika kuna joto jingi linaloambatana na wadudu wanaoathiri mimea. Mimea inayopatikana kwenye maeneo yanayozingira ikweta pia huwa na viwango vya chini vya madini kushinda inayokuzwa kwenye joto la wastani.

Maisha ni magumu zaidi katika mataifa yenye viwango vya juu vya joto. Kulingana na Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Hali ya Anga IPCC, Afrika itakumbwa na athari kali zaidi kutokana na mabadiliko ya hali ya anga ikilinganishwa na Uropa. Hatuwezi, kwa kiwango chetu, kutumia masharti yanayotolewa na wahifadhi mazingira wa Uropa. Inapohusu mabadiliko ya hali ya anga Afrika inaning'inia hatarini, Uropa iko tayari.

Hoja nyingine ya kupotosha inayotolewa dhidi ya mimea ya GM inayohusu kulinda mimea ya kiasili. Vyakula vyetu ni mchanganyiko wa kimataifa. Chakula chetu cha kimsingi, mahindi, yaliletwa na Wareno kutoka kwa Waamerika. Viazi na nyanya zinatoka kwa milima ya Ande. Mihogo, njugu, parachichi, mapera, viazi vitamu, mananasi na karakara zote ziliiletwa nchini kutoka Amerika Kusini.

Hofu ya mimea ya GM kwa kuwa soko linatawaliwa na mashirika ya kimataifa ya Amerika pia haina msingi. Fikiria kuhusu magari. Kama, kwa mfano, unalalamika kuwa moja kati ya Toyota na Volkswagen inashikilia robo ya soko, suluhisho haliwezi kuwa kupiga marufuku magari yote.

Tunahitaji mimea inayoweza kustahimili kiangazi kwa njia bora zaidi, inayohitaji kiwango cha chini cha dawa za kuangamiza wadudu, inayozalisha kiasi cha juu cha virutubisho na kupunguza athari zinazosababishwa na kilimo kwa mazingira.

Rais Ruto ni sharti ahakikishe kuwa ndiye rais wa mwisho kuwahi kuzindua rasmi usambazaji wa chakula cha msaada.

*Bw Odongo ni Mhandisi wa Datakazi* ***wagaodongo@gmail.com***
*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

Nation Media Group "ePaper Copy"

SEKTA YA MAVAZI

# HAPA NI MITINDO HALI YA JUU

**NI WAKATI WA YUVA YA AFRIKA:** Kwa kujumuisha utaalamu na ubunifu, Mawia Muthengi amekuwa mwanamitindo wa watu maarufu, kuanzia mwigizaji Lupita Nyong'o, Gavana Anne Waiguru hadi familia ya aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta.

NA EDDY ASHIOYA

Tafakari haya. Umeketi ufuoni. Barobaro anayeitwa Alejandro anakutilia mvinyo maarufu kama Bloody Mary kisha anakutupia macho - na ninamaanisha macho yenu yanatazamana - na kuishia kuvizia misuli yake iliyochongeka kwa ustadi.

Ashiki ya Gumzo la Kusisimua inapanda kwa matao ya chini katika mwanga wa jua linaloangazia paa la hoteli ya watu mashuhuri katika eneo la kifahari lisilo na jina.

Hiyo ndiyo taswira aliyo nayo Beverly Mawia Muthengi kuhusu adhuhuri kamili.

Hautalaumiwa kwa kukosa kufahamu Mawia Muthengi ni nani, au mambo anayojali. Hadi nitakapokujuza kuwa anaendesha African Yuva, kituo cha kuuza mavazi yanayoegemea mitindo na bidhaa za Kiafrika. Bado hujashawishika? Vipi nikikueleza kuwa amemvisha kila mtu katika tasnia hii? Orodha yake ndefu ya vigogo maarufu inajumuisha mwigizaji aliyeshinda Tuzo ya Oscar, Lupita Nyong'o, Gavana wa Kirinyaga Anne Waiguru na watoto wa Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta katika harusi yao (Jomo Kenyatta na Fiona Achola).

Aidha, ameunda mitindo ya waigizaji wa filamu kadhaa za Netflix ikiwemo Single Kiasi (nyingine zinakuja na kutokana na Mikataba yake inayozingatia Faragha, hatuwezi kufichua zaidi). Mtangazaji bidhaa mitandaoni, Murugi Munyi, msanii wa nyimbo za injili Kambua, mtaalamu wa mawasiliano, Lucia Musau, mwanahabari maarufu, Grace Msalame na waundaji matini Patricia Kihoro na Sharon Mundia pia wamejua uwezo wa sindano yake.

"African Yuva ilianza kama uraibu niliokuwa nikishiriki kujifurahisha. Nilipoanza, hakukuwa na nembo nyingi za Zimeundwa Kenya, kando na mafundi wa humu nchini na duka za magora eneo la River Road. Enzi hiyo, mafundi sawa na hulka yao ya mafundi, walitamausha wateja na kutoweka na magora yao au kuwaundia vitu vyao binafsi. Hapo ndipo African Yuva ilizaliwa - ahadi yetu ni rahisi: unachoagizia ndicho unacholetewa."

Na ni kweli. Kwa sababu kila mtu ambaye amefanya kazi na mafundi anajua, huwa wanakufunza subira. Kuwa na almasi na dhahabu ni jambo zuri, lakini fundi wa kuaminika nani anaweza kumpata?

Fundi wako awe ametoka Mombasa au Maralal. "Mwanzoni, nilikuwa zaidi kama wakala. Nilikuwa nawapa kazi mafundi kulingana na walivyohitajika, na tungekuwa na mkataba, lakini tena, wangekosa kutimiza."

African Yuva ilianzishwa 2018, huku Mawia akijitokeza kikamilifu na kukusanya timu. Mnamo Oktoba, 2020, wateja wake waliongezeka na akafungua duka eneo la Ngara ambako alianza na mafundi wawili na msaidizi mmoja.

Kwa sasa, African Yuva ina mafundi wanne na wasaidizi watano. "Yuva" inamaanisha 'nyumbani' kwa lugha ya Kituruki. Hivyo basi, African Yuva inamaanisha Nyumbani kwa Mitindo ya Kiafrika.

Mawia, 26, ambaye ana shahada ya Uchumi na Takwimu kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi, amepitia panda-shuka zake katika jukwaa la biashara. Biashara huanza katika hali ya kubahatisha hadi unapotulia na kuchukua mkondo wako. Kwake, imekuwa wanawake. Kwa nini wanawake? "Wanawake daima hununua nguo na isitoshe, mimi ni mwanamke na naelewa kile wanawake wanataka kuvaa. Idadi kubwa ya mavazi yangu yanaweza kuvaliwa na watu wote kuanzia wembamba hadi wanene."

"Ninachukia kumlipisha mtu zaidi kwa kuwa mnene. Ni kweli, kitambaa kikubwa zaidi kitatumika, lakini kidogo kitatumika pia kwa mtu mwingine. Mbona usipate njia ya kuelewana?" Mteja wake halisi ni mtu anayetaka kuvutia. Na muhimu zaidi, asiwe na tatizo kugharamia vazi bora. Anasema haya akiwa na hakika, ambapo mitindo yake ya magauni hufikia hadi Sh25,000.

Mitindo ya Kiafrika ni maarufu leo. Kila kunapokuwa na kongamano kuhusu Afrika barani Afrika, itakuwa vigumu kukosa mtu aliyevalia mitindo ya Kiafrika. Hakuna ajuaye au anayeweza kusema vazi la Kiafrika ni gani, au linafanya kazi vipi. Lakini bado huwa linaibua hulka ya aina yake ya kuvutia. Kuna soko la mitindo iliyoundwa Afrika. Mavazi yangu ni ya hali ya juu. Huwa tunawatunza wateja wetu nao hurudi tena na tena."

"Aghalabu, huwa ninaunda kile ambacho mimi mwenyewe naweza kuvaa. Hata kabla ya kuzindua nembo, huenda nitakuwa tayari nimevalia vazi hilo na kuamua iwapo litapendeza kwa watu wengine."

Mitindo pia inahusu ladha ya kidhahania. Si kila mara ambapo mchuzi mtamu kwa bata jike huwa mtamu pia kwa bata dume. Ndiposa nataka kujua, ni kipi watu hukosea kuhusu mavazi? "Ni katika kuvalia au uundaji? Upande wa kuvalia bila shaka. Anatafakari kwa muda - kwa dakika "Zingatia kuhusu kuchanganya rangi kwa mfano. Watu sasa wanaweza kuvalia rangi ya zambarau na nyekundu na bado wavutie." Ngoja kidogo, zambarau na nyekundu? Ninasitasita. "Naam! Kwa hakika siwezi kufanya hivyo, ni sharti uwe mwangalifu kuhusu hilo. Huwezi tu kuchanganya rangi zozote eti mitindo imebadilika." Ninajikumbusha hatimaye



Beverly Mawia anamiliki African Yuva, duka la kuuza mavazi ya wanawake yanayoegemea mitindo na bidhaa za Kiafrika.
PICHA | JEFF ANGOTE

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



Beverly Mawia na wafanyakazi wake katika duka la African Yuva, eneo la Ngara, jijini Nairobi, mnamo Oktoba 12. JEFF ANGOTE I NATION



Beverly Mawia katika duka lake jijini Nairobi. JEFF ANGOTE I NATION



Moja la mavazi ambayo African Yuva ilimuundia mshindi ya tuzo ya Oscar Lupita Nyong'o.

kujitokeza kwa kishindo nikiwa nimejikwatua kwa surupwenye yangu nyekundu na shati ya zambarau – Vazi Bora la Jumapili. Mitindo, sawa na mapenzi na lugha, ni jambo linalobadilika.

Lilian, ambaye ni "mteja sugu anayerudi kila mara" jinsi anavyopenda kujiita, anachangia mdahalo huu. "napenda African Yuva na kaulimbiu ya nembo yake. Nimenunua surupwenye kadhaa aina ya Palazzo kutoka kwa Mawia na jinsi kila kitu kinavyotoshea kwa ukamilifu wa kupigiwa mfano utafikiri wanauza zilizoundwa-kutoshea."

Unapozungumza na Mawia unapata hisia ya Kuhani Mkuu wa fmitindo - bado hajafikia kiwango cha Anna Wintour lakini anakaribia hapo - kielelezo cha maadili ya juu zaidi ya mitindo, mchanganyiko wa ladha zake maridadi, shabiki mkuu wa mavazi ya kisasa, anayezidi kuongoza African Yuva kwa shauku badala ya kulazimisha.

Ni mtindo gani ambao hawezi kukosa kila siku? "Ukakamavu." Lahaula! Ni mtani kupindukia. Pengine ninachohitaji tu kujitokeza kwa shati yangu ya zambarau na surupwenye nyekundu ni ujasiri?

"Ninachopenda kuhusu Mawia ni utaalamu wake," anasema Lilian. Akisema atakamilisha katika wakati fulani, anafanya hivyo kwa wakati huo. Na ana sauti hii nzuri yenye ukarimu, ni furaha kubwa kufanya kazi naye."

Mwanamitindo nyota Brian Babu anakubaliana na hili. "Sanaa yao (African Yuva) ni ya Kiafrika na imeundwa kwa njia bora. Navutiwa na jinsi wanaibua biashara ya ubunifu ya Kenya na Afrika kwa jumla. Navutiwa hasa na jinsi wanavyomalizia suruali ndefu, ambazo pia hupigwa uzi kwa njia maridadi kabisa. Lakini ninachopenda zaidi kuhusu Mawia ni kuwa ana namna ya kipekee ya kuhudumia wateja na huwa anawahudumia upesi."

Kama mtaalamu jinsi alivyo, Mawia anafikiri nini kuhusu kinachosemwa na mavazi yetu? Anaanza kwa msemo maarufu kwamba "valia jinsi unavyotaka kuchukuliwa." Watu hutambua vitu. Wanawake hasa huona viatu. Huwa pia wanaona ukakamavu, hivyo basi wewe pia unapaswa kufanya hivyo. Kisha anaendelea kuchambua mtindo wangu wa mavazi, kijisehemu hadi kingine, ambao kwa sababu ya hadhi yangu sitachapisha hapa.

"Kama mfanyabiashara chipukizi, huwa nashangaa iwapo najitahidi vya kutosha kutosheleza wateja wangu. Mitindo yangu inakua kwa kasi ya kutosha? Huwa anajiliwaza kwa njia gani? "Ninapenda kupika vyakula vya Jumapili. Na hivi majuzi nilijiunga na gym!" Kuna kitu ambacho hakiwezi kabisa? "Mimi ni mzuri sana kwa kuwa mchezaji densi mbaya." Utani wa hali ya juu tena. "Wakati mwingine kujitetea binafsi na kile ninachotaka inaweza kuwa vigumu."

Kama leo ingekuwa mwisho wa kila kitu, ungependa kukumbukwa kwa lipi? "Utu wangu. Ningependa kukumbukwa kama mtu mkarimu kwa kila mtu niliyetangamana naye." Akitazama nyuma alikoanzia, je, anafikiri amefanikiwa kutokana na maarifa au ni bahati tu? "Mimi ni mtu mwenye maarifa na bidii. Nimefanya kazi kwa bidii kwa yote niliyofanikisha." Na kwa kauli hiyo, ni gharama ipi amelazimika kulipia kwa ufanisi wake? "Mahusiano machache ya kibinafsi huenda yamezorota kutokana na na hali yangu ya kuwa na shughuli nyingi. Isitoshe, sina muda na nafsi yangu tena. Najifunza kusambaza mamlaka ya usimamizi, kujitengea muda wangu binafsi. Unajua watu wanaosema ukifanya kitu unachopenda hutawahi kuhitajika kufanya kazi siku yoyote maishani mwako. Huo ni uongo. Napenda kufanya hivi, lakini asikudanganye yeyote; hii bado ni kazi," anasema.

"Africa Yuva ndilo pendo la maisha yangu. Ndiyo ninayolalia na kuamkia." Unajua jinsi kanga na leso hizo fupi za Waswahili zinavyoandikwa misemo. Kama yake ingesema kitu, kingekuwa nini? Anawaza kwa dakika nyingine mbili unusu. Naweza kukutumia ujumbe kwa simu? Bila shaka.

Baadaye usiku, ananiandikia ujumbe: Sisi ni mabinti wa wanawake waliotueleza tunaweza kuwa chochote tunachotaka kuwa na tukasikia," "Ni sharti uwe kila kitu unachoweza kuwa." Kauli ndefu sana, lakini ana vazi lake. "Kama ni ndefu sana," ujumbe wake unawasha mwanga wa kioo cha simu yangu sekunde chache baadaye - kana kwamba anasoma mawazo yangu - tunaweza tu kuandika, "Nilienda Alliance".

*eddyashioya@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

VITA VIKALI KUHUSU WATAZAMAJI

# PESA TELE MITANDAONI

• NA SINDA MATIKO

**MTANDAO WA KIJAMII:** Huku tasnia za mitandao ya kijamii ziking'ang'ania watazamaji na uaminifu wa waundaji matini, wauzaji bidhaa wana njia zaidi za kufikia wateja, nao watangazaji wa bidhaa mitandaoni wakijaza akaunti zao za benki

Ulimwengu ulibadilika kabisa wakati TikTok ilipozinduliwa mnamo 2016. Kufikia sasa, ndio mtandao wa kijamii unaokua kwa kasi zaidi nchini Kenya na duniani kwa jumla huku ukizidisha makali ya kumenyana na washindani wakuu Instagram, Facebook, YouTube, Snapchat na Twitter.

Hali hii imewapa wanaobuni matini na watangazaji bidhaa namna mbalimbali za kukamua hela. Huku ikiwa na watumiaji zaidi ya bilioni moja kila mwezi, TikTok imejigeuza kuwa moja kati ya tasnia muhimu zaidi za matangazo ya kibiashara kimtandao leo hii.

Katika juhudi za kuvutia tena waundaji matini waliohama na kushawishi waliopo kuendelea kukaa, mitandao yote ya Instagram, Facebook, YouTube na Snapchat imeanzisha tasnia zinazoiga TikTok na zinasambaza mamilioni kama chambo cha kuwavutia kurudi.

Snapchat hutoa Sh120 milioni kila siku kwa video inayosambazwa mno kote duniani kwenye mtandao wake unaoiga TikTok, kwa jina Spotlight, uliozinduliwa mnamo Novemba 2020.

YouTube ina mtandao wake unaoiga TikTok wa YouTube Shorts, uliozinduliwa Septemba 2020, ambao unatoa Sh12 bilioni ambazo waundaji matini kote ulimwenguni, ikiwemo Kenya, wanaweza kushiriki.

Mapema mwezi huu, mitandao ya kijamii ya kampuni ya Meta, inayomiliki Facebook, Instagram na WhatsApp, ilitangaza kuwa imepanua mpango wake wa kuunda hela kwa mataifa 150 duniani, ikiwemo Kenya, katika tasnia zake za Instagram Reels na Facebook Reels, zilizoanzishwa Agosti 2020 na Septemba 2021 mtawalia. Wasanii wa Kenya sasa wanaweza kuunda kiasi kikubwa cha hela kutokana na mpango wa Reels Play Bonus, unaofadhiliwa na hazina ya muundaji ambayo ni Sh120 bilioni.

Hii ina maana kuwa waundaji matini, wanaojumuisha wasanii maarufu na watangazaji bidhaa mitandaoni hawatahitaji tena kutegemea uundaji matini kwa bidhaa na kampeni za ufadhili; wanaweza pia kujinufaisha kupitia malipo ya Reels kutokana na jinsi matini yao inavyosambazwa. Mpango wa malipo ya bonasi utategemea yatakayofanyika kwenye filamu hiyo fupi - Reels (kutazamwa, kubonyeza like, kuchangia na kutajwa).

TikTok binafsi ilizindua hazina ya Sh24 bilioni mnamo 2020 lakini iliyolenga tu waundaji matini walio Amerika. Hata baada ya uzinduzi wa hazina mbalimbali za washindani na waundaji, ambazo zimo katika hatua zake za kwanza Kenya, mtandao huo umeendelea kuwa maarufu nchini. Muundaji matini Azziad Nasenya, 22, aliyejipatia umaarufu mnamo 2019 kutokana na video yake ya sekunde 15 iliyotamba mno TikTok, bado anapendelea apu hiyo.



Shabiki wa TikTok Azziad Nasenya

"TikTok ina kila kitu ninachohitaji. Naweza kuiga sauti, kuigiza, kusakata densi na kuunda video za kuchekesha. Inawezesha yote hayo kufanyika. Ni mtandao unaokuruhusu kuwa wewe halisi kwa sababu ni nadra utukanwe kwenye mtandao huo hivyo kumpa mtu uhuru wa ubunifu na uhalisia," anasema Azziad aliye na zaidi ya wafuasi 2.2 milioni kwenye apu hiyo, 1.7 milioni Instagram, 565,000 Facebook, 232,000 Twitter na 169 kwenye YouTube.

Hata hivyo, video zake kwenye Instagram Reels zinaonekana kuwa na kasi zaidi ya kusambazwa kuliko TikTok. Kwa mfano, video aliyochapisha majuzi ya kutangaza bidhaa mojawapo ya Maybelline ilivutia utazamaji mara 384,000 kwenye Instagram Reels katika muda wa siku nne ikilinganishwa na utazamaji mara 51,000 kwenye TikTok. Huwa anapigia debe bidhaa mbalimbali kwenye mitandao yake ya kijamii kwa kuzingatia ni upi unaopendelewa na wateja wake.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

Azziad ni mwigizaji maarufu katika vipindi mbalimbalib vya televisheni humu nchini lakini sehemu kubwa ya mapato yake inatokana na utangazaji wa bidhaa mitandaoni, ambapo hulipisha kiasi cha hadi Sh500,000 kwa kampeni za kupigia debe bidhaa na Sh30,000 kutaja bidhaa.

Alma Mutheu, muundaji matini aliye na shahada ya digrii katika Kiingereza na Fasihi anashukuru Instagram na TikTok kwa kumpa sehemu kubwa ya mapato yake. Hata hivyo, anapendelea TikTok kwa sababu ya muundo wake. "Kila moja ni tofauti kivyake, lakini nikitakiwa kuchagua moja, nitachagua TikTok kwa sababu ina ushirikishi zaidi. Inachangamsha, ni rahisi kuunda matini na ina aina nyingi za sauti zinazoweza kuchaguliwa. Aidha, nahisi ni rahisi sana kukua kwenye mtandao huo: Nina wafuasi kutoka nje ya nchi, ikiwemo Amerika lakini ni vigumu kufanya hivyo kwenye Instagram kutokana na jinsi muundo wake umepangwa." Mutheu hupata kati ya Sh30,000 na Sh100,000 kutegemea na aina ya kandarasi aliyopewa ya kutangaza bidhaa.

Brian Mutinda, mwandishi wa nakala za mashirika na mtangazaji bidhaa mitandaoni, ambaye umri wake unakaribia miaka 30, anapendelea kuunda hela zake kwenye Instagram, ambapo ana wafuasi 105,000 ikilinganishwa na 18,500 kwenye TikTok na 134,000 kwenye Twitter. Mutinda hutumia kati ya dakika 30-50 kwenye mitandao ya kijamii kila asubuhi kama shughuli yake ya kwanza ya siku. "Huwa naingia Facebook, Twitter, TikTok, Instagram na Telegram kutazama mikondo na kujifahamisha kuhusu masuala ibuka. Inanipa maarifa kuhusu ni aina gani ya matini ninayopaswa kuunda kwa siku hiyo."

Ingawa wakati mwingine huwa anachapisha matini katika tasnia zake zote, mara nyingi huziunda kwa njia mahsusi kutegemea mtandao husika, akipendelea Instagram. "Nahisi inavutia zaidi kwa sababu ya mwonekano wake na ina ushirikishaji zaidi matini inapoundwa ipasavyo. Muundo wa Instagram hutoa kitengo maalumu cha hadhira iliyo na mawazo sawa, sifa muhimu kwa kazi ninayofanya, kinyume na TikTok, ambayo ni pana," anafafanua Mutinda.

Mchekeshaji aliyegeuka kuwa muundaji matini, Eddie Butita, ambaye ni mwanzilishi wa kampuni ya mtandao kwa jina Stage Presence Media Limited, hana mtandao anaopendelea ingawa ana wafuasi wengi kwenye Instagram wasiopungua 483,000 wafuasi 63,000 kwenye TikTok, 506,000 kwenye Facebook na 167,000 kwenye Twitter. Msanii huyo mwenye umri wa miaka 29 hutoza kuanzia Sh200,000 kutangaza bidhaa mitandaoni. "Mitandao yote hiyo inaweza ikakunufaisha mradi tu uelewe lugha zake. TikTok humpa msanii fursa pana ya kutangamana na hadhira mpya, huku Instagram ikihusisha mahali ulipo, unachokula na mambo kama hayo. Facebook ni kukuhusu wewe binafsi na hadithi unazosimulia watu, huku TikTok ikihusu burudani pekee.

"Kwa muda mrefu Facebook imekuwa ikiepukwa na watangazaji bidhaa mitandaoni lakini mimi huona ikiwa na uwezo mkubwa kwa sababu ina baadhi ya viwango vya juu zaidi vya usambazaji. Lakini nakubali kuwa TikTok ndio mtandao uliobobea zaidi. Haujakuwepo kwa muda mrefu lakini athari yake imekuwa kuu.," anasema Eddie.

Kukwea kwa TikTok hadi kilele cha tasnia ya mitandao ya kijamii kumeibua msisimko mkubwa hasa baada ya kutawaliwa na washindani wake kwa miaka mingi. Licha ya kupumbaza Kizazi cha kiasasa maarufu kama Gen Z, TikTok haikupaa kwenye upeo kwa usiku mmoja. Ilianza kwa kuvutia kizazi cha vijana na kujikuza hadi kufikia wazee.


Sababu rahisi kuhusu ni kwa nini watu wanazidi kufurika TikTok ni muundo wake wa kipekee na, kwa kinaya, njia mufti ya kupoteza wakati.

Mnamo Septemba 2021, TikTok ilifichua kuwa ilikuwa na watumiaji zaidi ya bilioni moja kila mwezi, idadi inayokadiriwa kuwa imepanda hadi karibu 1.6 bilioni kufikia mwisho wa Machi. Huku TikTok ikiwa imepanua muda wa video zake kutoka sekunde 15 hadi dakika 10, apu hiyo iligeuka mshindani hatari dhidi ya YouTube. Hata hivyo, bidhaa ambazo zimetamba kupitia kampeni za TikTok huenda zikapata matokeo hayo si lazima yajitokeze kwenye YouTube Shorts.

"Kizazi cha watu wazee wanapendelea zaidi YouTube Shorts ikilinganishwa na Gen Z, hivyo basi ujuzi unaojifunza kwenye TikTok huenda usitumike vyema katika YouTube Shorts," anasema Joshua DuBois, mkurugenzi wa shirika la utafiti wa soko kwa jina Gauge. Apu hizo hazishindanii tu watumiaji, bali pia mapato ya matangazo. YouTube ilizalisha Sh3.4 trilioni kama mapato ya matangazo mnamo 2021 ikilinganishwa na TikTok iliyopata Sh480 bilioni, kiasi ambacho kitaongezeka karibu mara tatu kufikia Sh1.4 trillion.


Huku tasnia za mitandao ya kijamii ziking'ang'ania watazamaji na uaminifu wa waundaji matini, wauzaji bidhaa wana njia zaidi za kufikia wateja, nao watangazaji wa bidhaa mitandaoni wakijaza akaunti zao za benki

***tmatiko@ke.nationmedia.com***




ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

taharirI




■ Ni miongoni mwa Warusi wengi wanaoamini kugawanywa kwa USSR kulikuwa makosa

# Putin amejitolea kurudisha Muungano wa Sovieti



KWENDO OPANGA

Ulimwengu unafaa kujua Urusi haitakoma kufanya kile imepanga kufanya, ikiwemo kutumia wanajeshi wake kushambulia jirani zake, eti kwa kuwa Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Amerika, Umoja wa Ulaya (EU) zimeionya dhidi ya kufanya au zimeilaumu kwa kufanya hivyo.

Rais Vladimir Putin ni miongoni mwa Warusi wengi wanaoamini kuwa kugawanywa kwa Muungano wa Sovieti kulikuwa makosa. Putin ameripotiwa na shirika la habari la "World Is One News" akitaja kusambaratika kwa USSR kuwa makosa makubwa ya kihistoria kuwahi kutokea katika karne hii.

Mwezi jana, Putin alionekana kwenye televisheni akisimama peke yake kando ya jeneza la kiongozi wa mwisho wa USSR, Mikhail Gorbachev. Alisimama kwa muda, akagusa jeneza, akatazama picha ya mwendazake kisha akaenda zake.

Taarifa rasmi zilisema Putin hakuhudhuria mazishi ya Gorbachev kwa kuwa alikuwa na shughuli zingine. Ripoti zingine zinasema alimtembelea hospitalini kama ishara ya kutoa heshima zake za mwisho.

Putin ni miongoni mwa wengi nchini Urusi ambao walimlaumu Gorbachev na sera zake za glasnost (uwazi) na perestroika (mageuzi) wakidai ndizo zilichangia kuporomoka kwa USSR mnamo 1991. Gorbachev alipendwa sana na viongozi wa mataifa ya Magharibi na hii ndiyo maana Putin alikataa kuungana nao katika mazishi yake.

**Mnamo 2014, Urusi ilituma wanajeshi katika eneo la Crimea, linalotambuliwa duniani kuwa chini ya Ukraine. Baada ya kupiga kura ya maamuzi, iliteka eneo hilo na kulitangaza kuwa sehemu ya Urusi.**

Kuhusu uvamizi wa Ukraine, itaonekana kuna mpango uliowekwa na Urusi mnamo 2008. Wakidai kulikuwa na mauaji ya halaiki katika maeneo ya Abkhazia na Ossetia, wanajeshi wa Urusi walivamia Georgia na kudhibiti maeneo hayo mawili. Bunge la Georgia, liliitaja Warusi kuwa watekaji maeneo.

Mnamo 2014, Urusi ilituma wanajeshi katika eneo la Crimea, linalotambuliwa duniani kuwa chini ya Ukraine. Baada ya kupiga kura ya maamuzi, waliteka eneo hilo na kulitangaza kuwa sehemu ya Urusi. Serikali ya Urusi ilidai wanamgambo wa Ukraine walitishia maisha ya wakazi na vituo vyake vya kijeshi.

Miezi saba iliyopita, wanajeshi wa Urusi walivamia Ukraine kwa sababu serikali ya nchi hiyo ilidai Ukraine ilikuwa ikijihusisha na vitendo vya mauaji ya halaiki dhidi ya wakazi wa eneo la mpakani. Urusi pia ilionekana kukasirishwa na hatua ya Ukrane kujiunga na Shirika la North Atlantic Treaty Organisation (NATO). Ilidai kuwa hatua hiyo ilikuwa ni sehemu ya Ukraine kuweka pamoja zana hatari za kivita kwa lengo la kuivamia.

Serikali ya Urusi ilipinga kabisa hatua ya taifa hilo, ambalo zamani lilikuwa sehemu ya USSR, kujiunga na NATO. Inachukulia hatua hiyo kuwa sehemu ya mpango wa mataifa ya Magharibi kuiweka hatarini kwa kuendeleza ushawishi wake hadi Ukraine. Makubaliano miongoni mwa mataifa wanachama wa Nato ni kuwa kushambulia mmoja ni sawa na kushambulia wote. Mwanachama wa Nato aliye karibu na mpaka wa Urusi (Ukraine) ndiye anachukuliwa na serikali ya Urusi kuwa adui.

Kufikia sasa Urusi imeonekana kuweza kustahimili vikwazo ilivyowekewa na mataifa ya Magharibi. Isitoshe, imeonekana kulipiza kisasi kwa kusitisha usafirishaji wa gesi hadi mataifa ya Uropa kando na kulazimisha mataifa hayo kulipia gesi hiyo kwa sarafu yake ya rouble. Urusi pia imeungana na nchi za China na Saudi Arabia kuhujumu thamani na hadhi ya dola ya Amerika ulimwenguni.

Urusi inajua hatua ya kukatiza usambazaji wa gesi hadi Uropa na kusisitiza ilipwe kwa sarafu ya rouble itavuruga bara hilo.

Shambulio la makombora dhidi ya miji 10 ya Ukraine mnamo Jumatatu lilithibitisha kuwa Urusi bado imejitolea kuisambaratisha Ukraine kwa njia zozote zile. Putin anataka ushindi nchini Ukraine. Anaambia mataifa ya Magharibi yakae kando.

*kwendo58@gmail.com*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

■ Kwa vyovyote vile DPP atakuwa na wakati mgumu kuhalalisha hatua yake ya kuondoa kesi

# Chungeni laini zenu jamaa, kuna bosi mpya jijini



MACHARIA GAITHO

Uamuzi wa Mahakama Kuu ulioidhinisha kufungwa jela kwa Mbunge wa Sirisia John Waluke na mshirika wake Grace Wakhungu, dada ya aliyekuwa Makamu Rais Moody Awori, bila shaka ulikuwa ufanisi mkubwa katika vita dhidi ya ufisadi.

Uliondoa mtazamo kwamba kesi zote dhidi ya watu matajiri na wenye nguvu huporomoka kutokana na ufisadi na njama ndani ya mfumo wa kutafuta haki wa kesi za uhalifu. Kifungo cha miaka 67 jela na faini za karibu Sh1 bilioni kila mmoja ni za kwanza za juu katika nchi ambayo kuachiliwa huru kufuatia kuvurugwa makusudi kwa uchunguzi na uendeshaji mashtaka ni kawaida. Hata katika kesi ambazo watu hupatikana na hatia, washtakiwa hupewa hukumu ndogo, mara nyingi faini ya chini kuliko walichoiba.

Mahakama Kuu iliidhinisha hukumu hizo siku ambayo ilibatilisha kuachiliwa huru kwa aliyekuwa Mbunge wa Kipipiri Amos Kimunya na ikaagiza kesi yake tofauti ya ufisadi iendelee. Ni muhimu kutambua kuwa, katika maamuzi hayo ya Mahakama Kuu, hapakuwa na malalamishi ya kawaida kutoka kwa wanasiasa.

Kilicho hakika ni kwamba kama Waluke, Wakhungu na Kimunya wangekuwa wamehusishwa na muungano wa Kenya Kwanza, washirika wao wangekuwa wamewaka moto, wakidai ni dhuluma na mateso yanayolenga wafuasi wa Rais William Ruto.

Wote wanaojificha chini ya magwada ya Ruto wanapopatikana wameiba mali ya umma, na makosa mengine mabaya ya uhalifu, yakiwemo mauaji na ubakaji, wangekuwa wanaongoza lawama dhidi ya polisi, waendesha mashtaka na majaji.

Wangekuwa wanarusha lawama huku wakitoa kila aina ya vitisho ambavyo vinahujumu pakubwa mfumo wa haki katika kesi za uhalifu, na bila shaka wakiapa kwamba kwa vile sasa wako mamlakani, washirika wao wote wangeachiliwa huru, maafisa waliohusika kufutwa kazi na kugeuza vita kwa wapinzani wao wa kisiasa.

Ingekuwa bora kuota na kufikiria kuwa siku zijazo, mahakama zingeonyesha moyo kama huo katika kuamua kesi nyingi zilizorundikana, zikiwemo zinazoathiri matajiri na wenye nguvu katika muundo wa mamlaka wa Ruto. Hata hivyo, tunapiga hatua moja mbele na tatu nyuma.

Katika wiki iliyopita, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma Noordin Haji aliondoa kesi kadhaa za ufisadi, baadhi zilizohusu watu mashuhuri katika msafara wa Ruto. Kesi ya ufisadi uliyohusu Sh19 milioni dhidi ya Waziri Mteule wa Utumishi wa Umma, Aisha Jumwa iliondolewa bila maelezo ya kuridhisha.

Ni afueni iliyojiri wakati unaofaa kwa kuwa mbunge huyo wa zamani wa Malindi anajiandaa kupigwa msasa na Bunge ambapo masuala ya maadili bila shaka yangeibuka. Hata hivyo, bado kuna kesi ya mauaji dhidi yake. Wengine walionufaika na hatua ya Haji kwa usajari ufuatao ni aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Kenya Power, Ben Chumo na washtakiwa wenzake 10 na aliyekuwa Gavana wa Samburu Moses Lenolkulal.

Haji pia alitangaza kuondoa mashtaka dhidi ya watetezi wa haki za binadamu na wanaharakati kadhaa waliokamatwa wakati wa maandamano tofauti katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita.

Nyingi za kesi hizi ziliondolewa bila hata "kuomba radhi", lakini zinaweza kuzua maswali ambayo yanaweza kufanya maamuzi ya Haji kupigwa darubini.

Kama iliamuliwa hakukuwa na ushahidi wa kutosha kuhalalisha kuendelea na kesi, basi Haji lazima aeleze ni kwa nini walishtakiwa. Baadhi ya walioachiliwa huru wamepewa sababu za kutosha kushtaki serikali kwa unyanyasaji, vitisho, kupakwa tope, kupoteza biashara, na kitu kingine wanachoweza kufikiria kufyoza mlipa ushuru.

Kuondolewa kwa kesi hizo kunathibitisha madai ya wafuasi wa Kenya Kwanza kuwa wamekuwa wakidhulumiwa kwa sababu ya kumuunga mkono Ruto.

Hali nyingine inayoweza kuibuka ni kuwa si ukosefu wa ushahidi au sababu nyingine kuu, lakini huenda Haji anafanya hivyo kwa kulazimishwa, ikizingatiwa kampeni za Ruto za kumaliza kesi alizodai ni za ubaguzi au kwa hiari yake mwenyewe ili kujipendekeza kwa utawala mpya.

**Kilicho hakika ni kwamba kama Waluke, Wakhungu na Kimunya wangekuwa wamehusishwa na muungano wa Kenya Kwanza, washirika wao wangekuwa wamewaka moto, wakidai ni dhuluma na mateso yanayolenga wafuasi wa Rais William Ruto.**

Kwa vyovyote vile DPP atakuwa na wakati mgumu kuhalalisha kuondoa kesi kwa wakati na hali inayoingiliana vyema na matamanio ya serikali ya Ruto.

Taswira iliyojitokeza ni kuwa iwapo polisi, waendeshaji mashtaka, majaji, maafisa wa ushuru na wengine chini ya serikali ya Uhuru Kenyatta walilaumiwa kwa haki au kwa makosa, kutumiwa kisiasa na utawala huo, sasa watageuka digrii 180 kuhudumia bosi mpya.

Kuna kesi nyingi kortini zinazohusu washirika wa Ruto ambazo bado hazijaamuliwa na inasubiriwa kuonekana iwapo pia zitaondolewa. Kinachofuata sasa ni ahadi ya kuandama yeyote katika familia ya Uhuru na washirika wake wa kibiashara na kisiasa, ambao wanalaumiwa kwa kufilisisha serikali kupitia uporaji mkubwa unaodaiwa kupita ule wa serikali ya udikteta ya Daniel arap Moi. Hii itajiri kupitia rais kuteuwa tume ya kuchunguza utekwaji wa serikali au badala yake, kupitia kuanzishwa kwa uchunguzi na kushtakiwa kupitia mifumo iliyomo.

Idara ya Uchunguzi wa Uhalifu inatafuta mkurugenzi mpya kumrithi George Kinoti ambaye alisoma dalili na kujiuzulu punde tu Ruto alipoingia mamlakani. Hitaji muhimu la kuteuliwa ni lazima mtu awe mwaminifu kwa KK.

Tume Huru ya Maadili na kupambana na Ufisadi inayoongozwa na Twalib Mbarak imepatiwa onyo kwamba heri itambue serikali mpya, huku Haji katika Afisi ya DPP tayari akionekana kucheza ngoma.

Katika Mahakama, Mahakama ya Upeo imepongezwa na serikali mpya kwa uamuzi wa kutupilia mbali kesi ya kupinga matokeo ya kura ya urais.

Wakati huo huo wachanganuzi wengi, walikuwa wepesi wa kugundua heshima ambayo Jaji Mkuu Martha Koome alionekana kupatia Ruto wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge. Mfalme Amefariki. Mfalme Aishi Maisha Marefu!

*gaithomail@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ MATAMSHI YENYE UTATA

# ULIMI WAMSUMBUA 'RIGGY G'

● NA MACHARIA GAITHO

*Ulimi mwepesi wa Rigathi Gachagua na matamshi yake ya kiholela hadharani hatimaye yanaweza kumuonyesha kuwa kinyago wa kisiasa, asiyestahili wadhifa wa Naibu Rais na ambaye matamshi yake hayawezi kutiliwa maanani*

Naibu Rais Rigathi Gachagua anaungama kuwa kauli zake tatanishi zimezua tumbojoto, lakini anajisifu kuwa msema kweli, bila kujali athari zozote za kisiasa.

Wiki tatu zilizopita, kwenye mahojiano ya kwanza tangu ishike wadhifa huo, alikubali kuna watu ambao hawakufurahia yake katika Uwanja wa Michezo wa Kasarani, wakati wa kuapishwa rais, lakini akasisitiza kuwa haombi msamaha na ataendelea kuongea ukweli jinsi alivyofunzwa na wazazi wake.

Katika hotuba yake kabla ya kumualika Rais William Ruto kuhutubia Wakenya, Rigathi alimkashifu vikali Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta, aliyeketi kimya.

Wengi walimkosoa Rigathi kwa kurudia kauli za kampeni katika sherehe rasmi iliyohudhuriwa na karibu marais 20 wa Afrika, maafisa wa serikali na wawakilishi wakuu wa kutoka sehemu tofauti duniani.

Tangu wakati huo, Naibu Rais ameendelea kutoa kauli tata. Asipomshambulia moja kwa moja Uhuru au mshindani wa Ruto katika uchaguzi wa urais, Raila Odinga, anaingilia taasisi za umma kwa matamshi yanayolenga kuonyesha kuwa, kauli za Kenya Kwanza kuhusu wizi, usimamizi mbaya na hazina tupu ya kitaifa iliyoachwa na serikali ya awali.

Ametoa pia kauli kadhaa kuhusu ajenda muhimu za Kenya Kwanza, ambazo pia zimeleta utata na mkanganyiko kwa kukosa tofauti kati ya sera ya serikali na maoni ya mtu binafsi.

Uzuri wake ni kuwa amekuwa mkarimu kwa vyombo vya habari. Amekuwa maarufu katika mahojiano ya redio na televisheni kama vile NTV na Citizen TV, ambazo wakati wa kampeni zililaumiwa na muungano wa Kenya Kwanza kwa madai ya kuegemea upande mmoja wa kisiasa.

Shida inayotokana na matamshi ya Gachagua ilionekana wiki iliyopita, wabunge watatu walipodai kuwa mashirika fulani ya serikali yanamchimba Naibu Rais kwa kumkosoa hadharani kuhusu taarifa zake.

Maseneta Wahome Wamatinga (Nyeri), John Methu (Nyandarua) na Mbunge John Kagucia (Mukurwe-ini) waliambia wanahabari eneo la Mukurweini kuwa ni tabia mbaya kwa maafisa wa serikali kumkosoa hadharani Gachagua ilhali anazungumza kwa niaba ya serikali wanayohudumia.

Wabunge hao watatu kutoka eneo la Mlima Kenya, anakotoka Gachagua, walikuwa wakizungumzia taarifa za mwenyekiti wa shirika la Kenya Airways, Michael Joseph, Gavana wa Benki Kuu (CBK) Patrick Njoroge na Waziri wa Fedha anayeondoka, Ukur Yatani, kuhusu matamshi waliyohisi yalitokana na hali ya kupotoshwa au kutofahamu.

Walisisitiza kuwa Naibu Rais alizungumza kwa niaba ya serikali, huku wakitishia kuwaita bungeni wakuu hao wa mashirika kuhojiwa.


Wiki iliyotangulia, Seneta wa Nandi Samson Cherargei alikuwa amezungumzia jambo hilo, akiwalaumu wakuu wa mashirika ya serikali kwa kutompa Rigathi heshima anayostahili.

"Kwa mashirika yote ya serikali na maafisa wa serikali, komeni kumjibu Naibu Rais Gachagua kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari. Kuna majukwaa mwafaka ya kuwasilisha masuala ya serikali ili kuheshimu ofisi hiyo," akasema Seneta huyo.

Naibu Rais pia aliungwa mkono na mtu ambaye hakutarajiwa - aliyekuwa Mbunge wa Nyeri Mjini, Ngunjiri Wambugu, ambaye alikuwa miongoni mwa wanasiasa wa kwanza kumfanyia kampeni Raila katika eneo hilo.

Katika taarifa aliyotoa mnamo Oktoba 4, Wambugu, ambaye aliyesombwa na wimbi la Kenya Kwanza, alilaumu vyombo vya habari kwa kumlenga Naibu Rais kwa kumulika mambo yanayoweza kumharibia sifa. kwa kumsawiri vibaya. "Huwa pia anasema mambo muhimu mbali na uchezhi na mzaha wake. Lakini vyombo vya habari huangazia tu habari zinazotufanya tumchekelee," akasema.

Lakini pia alitoa tahadhari, akionya kuwa huenda matamshi ya Rigathi yakamweka kwenye mtego. "Huenda ukafika wakati ambao ataonekana kuwa kinyago wa kisiasa, asiyestahili wadhifa wa Naibu Rais (na anaelekea katika mtego huo). Katika miezi michache ijayo, hakuna mtu atakayetilia maanani matamshi yake," akaeleza.




ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya kenya



Naibu Rais Rigathi Gachagua akiwa jukwaani na wanafunzi wa Chuo cha Ufundi cha Kitaifa cha Kisii wakati wa Tamasha za 94 za Kitaifa za Muziki Kenya mjini Kisumu mnamo Septemba 23.
PICHA | ANTHONY NJAGI

Gachagua mwenyewe amelazimika kujitetea dhidi ya baadhi ya matamshi yake.

Alipolaumiwa baada ya kutangaza kuwa serikali itarudisha mpango wa watu kulima kwenye misitu, alidai alinukuliwa vibaya na vyombo vya habari ingawa matamshi yake yalinaswa kwa video.

Gachagua alianza kujitetea baada ya mwenyekiti wa KQ Michael Joseph kukanusha madai yake kuwa shirika hilo linakabiliwa na matatizo ya kifedha kutokana na usimamizi mbaya na "kutekwa na serikali" kupitia

kandarasi tata za kukodisha ndege zilizofaidi wachache.

"Nauli zao ndizo za juu zaidi barani Afrika na ndege zao huwa zimejaa lakini bado wanapata hasara. Tunajaribu kukabiliana na hali hiyo ya kutekwa na serikali ili kupunguza gharama ya shughuli za shirika hilo kuliwezesha kupata faida," akasema Gachagua majuzi, akihojiwa na Citizen TV.

Joseph alikanusha madai hayo, akisema shirika hilo linakodisha ndege kutoka kwa kampuni maarufu za kimataifa zinazosimamia mamia ya ndege zinazokodishwa kwa mashirika mbalimbali ya kimataifa ya ndege ulimwenguni.

Aliorodhesha idadi ya ndege za kukodisha zinazotumiwa na KQ na kupuuza madai kuwa shirika hilo linalipa pesa nyingi kupita kiasi kwa ndege hizo.

Hata hivyo, taarifa ya KQ iliepuka masuala ambayo yamezua utata kwa miaka mingi, hasa madai kuwa ndege za KQ hazipatikani moja kwa moja kutoka kampuni za kukodisha, lakini kupitia kupitia kampuni za watu.

Gachagua pia alikuwa amedai kupitia televisheni kuwa Kenya haina pesa za kutosha za kigeni. "Hata jana, tulikuwa na shida CBK kwa sababu tulipata hapakuwa na pesa za kutosha za kigeni kutuwezesha kuagiza mafuta," akasema.

Benki Kuu ilijibu mara moja kupitia taarifa, ikieleza kuwa serikali huwa haiagizi mafuta, hivyo haikuitisha pesa za kigeni ili kuagiza bidhaa hiyo.

Ilieleza kuwa waagizaji mafuta, ambao wengi wao ni mashirika ya kibinafsi, hupata pesa za kigeni kutoka kwa benki za kawaida wala si kutoka kwa CBK. "CBK hutoa pesa za kigeni kwa Serikali ya Kitaifa pekee, wala si mashirika ya kibinafsi. Hivyo, waagizaji mafuta hupata pesa hizo kutoka kwa benki za kawaida," ikasema CBK kwenye taarifa hiyo.

"CBK ina pesa za kigeni za kushughulikia hali yoyote ambayo huenda ikaibuka," ikaeleza taarifa hiyo na kukanusha madai ya baadhi ya benki na wafanyabiashara kuwa kiwango cha pesa za kigeni nchini kilikuwa chini sana.

Waziri wa Fedha anayeondoka, Ukur Yatani, pia alipata fursa ya kumkosoa Gachagua punde tu baada ya serikali mpya kuchukua uongozi. Kaatika sherehe ya kuapisha rais, Gachagua alidai walirithi hazina tupu ya serikali.

Baadaye aliambia NTV serikali ilipata Sh93 milioni pekee katika Hazina ya Kitaifa. "Hakuna pesa zozote katika nchi hii na tunaanza upya. Nimewaomba Wakenya wawe na subira kwani tuna mpango. Hata hivyo, matokeo yake hayataonekana haraka kwani tumepata hali ya uchumi ikiwa mbaya," akasema Gachagua.

Waziri alitaja madai hayo kuwa yaliyotokana na kupotoshwa au kutofahamu. "Serikali haikusanyi pesa na kuzihifadhi katika sehemu moja, kuziweka kwa mwezi mmoja na baadaye kuzisambaza baada ya miezi kadhaa au baada ya mwaka mmoja," akasema Waziri wa Fedha.

Alieleza kuwa pesa hukusanywa na kusambazwa kila siku kufadhili shughuli za serikali ikiwemo mishahara na mambo mengine muhimu. Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Upelelezi wa Jinai (DCI), Hamisi Massa, pia alilazimika kumkosoa Gachagua. Massa anaongoza idara hiyo kwa muda baada ya mtangulizi wake, George Kinoti kuondoka.

Akihutubia mkutano wa magavana, Gachagua aliwalaumu polisi kwa madai ya kuhangaisha viongozi waliochaguliwa kupitia idara hiyo kwa kuvamia nyumba na ofisi zao. Aliagiza DCI akome kuwaaibisha viongozi hao, kauli iliyoibua maswali, kwani ilioneka-na kumaanisha kuwa viongozi hao hawafai kuulizwa chochote hata wakivunja sheria.

Baadaye, kwenye kikao na wakuu wa taasisi huru za kikatiba, Massa alisema polisi wataendelea kufanya kazi yao bila kujali hadhi ya anayevunja sheria.

Ingawa hakumtaja Gachagua moja kwa moja katika kauli yake, baadhi ya vyombo vya habari viliripoti kuwa alikuwa akizungumza kuhusu Naibu Rais.

Hilo lilimuweka Massa mashakani na kulazimu ofisi yake kutoa taarifa ya kujitenga na ripoti hizo. "Ripoti za matamshi yanayodaiwa kutolewa na Naibu Waziri hazikutoka kwa Kaimu DCI wala huo si msimamo wake," ikasema taarifa hiyo. "Kwa hivyo, tungependa kusema kuwa Kaimu DCI hakumtaja wala kuzungumza kuhusu Naibu Rais wala afisa mwingine yeyote wa serikali, kwa hivyo habari kuu ya gazeti si ya kweli."

Tabia ya Gachagua ya kutoa kauli tata ilianza kuonekana wakati wa kampeni za Kenya Kwanza. Kauli inayokumbukwa sana ni aliposema kuwa Kenya Kwanza

Ingeshinda, mashtaka ya ufisadi yanayomkabili yangefutiliwa mbali na mahakama na Sh200 milioni zilizochukuliwa kutoka kwake kwa agizo la mahakama zingerudishwa.

Ni kauli iliyoonyesha ahadi ya Rais Ruto kukabiliana na ufisadi kuwa mzaha. Pia ilitilia shaka ahadi yake ya kutoruhusu idara muhimu kama polisi, DCI na Mahakama kutumiwa kisiasa.

Viongozi wengi wa Kenya Kwanza na mawaziri wateule wanaochunguzwa ama tayari waliopatikana na hatia kwa makosa mbalimbali ya uhalifu wamekuwa wakidai wanateswa kisiasa. Inasubiriwa kuonekana iwapo serikali ya Ruto

itaruhusu sheria kufuata mkondo wake au kesi hizo zitaanza kufutiliwa mbali. Huenda kauli za Gachagua zilionyesha mkondo utakaofuatwa.

'Darubini ya Wiki' ilijaribu bila kufaulu kumfikia Gachagua kutoa kauli yake kuhusu habari hizi. Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano ya Rais (PSCU)

aliahidi kutusaidia kumhoji lakini hakuwa amefanya hivyo kufikia wakati tulipoenda mitamboni.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# SELI ZA KUTOKA MAABARA ZACHEZA TENISI YA VIDEO



LONDON

Watafiti wametengeneza seli za ubongo katika maabara, ambazo zimejifunza kucheza mchezo wa tenisi wa miaka ya 1970 unaojulikana kama 'Pong' kupitia kwa video. Wanasema "ubongo huo mdogo" unaweza kuhisi na kujibu hali katika mazingira yake.

Kwenye makala aliyoandika katika jarida la Neuron, Dkt Brett Kagan wa kampuni ya Cortical Labs, anadai alitengeneza ubongo wa kwanza "wenye uwezo wa kuhisi hali ya mazingira" kupitia maabara ndani ya bakuli.

Watafiti wengine wanataja kazi hiyo kuwa "ya kufurahisha" ingawa wamepuuza seli hizo zina uwezo wa kuhisi mazingira. "Hiyo ndiyo fasiri bora tuliyoona inafaa kutumiwa kuelezea kifaa hicho," akasema Dkt Kagan.

"Kina uwezo wa kuchukua maelezo kutoka kwa kifaa cha nje, kuyatathmini na kutoa majibu kuyahusu kwa muda mfupi sana."

Bongo kama hizo zilitengenezwa mara ya kwanza 2013 kutafiti maradhi aina ya microcephaly, ambayo huhusisha hali ya mtu kuwa na ubongo mdogo sana. Pia, bongo hizo zimetumiwa katika masuala ya utafiti kuhusu ukuaji wa akili.

Hii ni mara ya kwanza kwa seli hizo kuunganishwa na kifaa cha nje, mara hii ikiwa mchezo wa video. Kundi hilo la watafiti lilikuza seli 800,000 za ubongo kutoka seli kubwa maalumu za mwili na baadhi kutoka vitoto vya panya. Baadaye waliunganisha ubongo huo mdogo na mchezo wa video kupitia viunganishi vya umeme. Baada ya hilo, seli hizo zilizalisha umeme zenyewe.

Ubongo ulijifunza kucheza mchezo huo kwa dakika tano. Ingawa ulikosea mara kwa mara, kiwango chake cha mafanikio kilikuwa kikubwa.

Kulingana na watafiti, ubongo huo haufahamu kuwa unacheza mchezo wa Pong kama ilivyo kwa binadamu kwani hauna hisi kama ya mwanadamu.

Dkt Kagan anatumai huenda tekinolojia hiyo ikatumiwa kufanyia majaribio matibabu ya matatizo ya akili kama vile maradhi ya Alzheimer. "Hili linatufungulia njia ya kufanya utafiti katika nyanja nyingine muhimu kwa kina."

Katika utafiti unaofuata, Dkt Kagan anapanga kutafiti athari za vileo kwa uwezo wa ubongo huo mdogo kucheza Pong. Ikitoa majibu sawa na ubongo wa mwanadamu, basi hilo litaadhihirisha umuhimu wa mfumo huo katika kufanya tafiti kwa masuala mengine muhimu.

Urejeleo wa Dkt Kagan kuhusu uwezo wa kuhisi wa ubongo huo unatofautiana na fasiri zilizo kwenye kamusi nyingi za masuala ya kisayansi.

Dkt Dean Burnett kutoka Shule ya Masuala ya Saikolojia ya Cardiff anapendekeza hali hiyo kuelezewa kuwa "mfumo wa kufikiria." "Kuna maelezo yanayopitishwa kutoka eneo moja, kutumiwa na hatimaye kusababisha mabadiliko fulani. Hivyo, mchakato huo unahusu 'mfumo wa kufikiria'," akasema.

Kuna uwezekano wa bongo hizo kuboreshwa zaidi utafiti unapoendelea. Hata hivyo, kundi la Dkt Kagan linashirikiana na wasimamizi wa maadili katika masuala ya kisayansi, kuhakikisha hawatengenezi ubongo wenye uwezo kama wa mwanadamu. Ni hali inayoweza kuzua masuala ya kimaadili katika sayansi.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# Mtalii wa angani kuzuru mwezi kupitia SpaceX

Mfanyabiashara Dennis Tito kutoka Amerika anapanga kuzuru mwezini pamoja na mkewe, Akiko, kupitia kampuni ya Space X. Mnamo 2001, Tito alikuwa mtu wa kwanza kujilipia pesa zilizohitajika ili kuzuru angani.

Safari yake itafanyika baada ya kampuni hiyo, inayomilikiwa na bwanyenye Elon Musk, kumaliza kutengeneza roketi kwa jina Starship. Kwanza, roketi hiyo itamsafirisha bwanyenye Yusaku Maezawa kutoka Japan. "Tangu kuzuru angani kupitia roketi, bado naendelea kutamani kufanya ziara kama hiyo tena. Msukumo huo ndio umenifanya kushiriki ziara hii mara nyingine," akasema Tito, 82.

Ziara hiyo imepangiwa kuchukua muda wa wiki moja, ambapo roketi hiyo itazunguka maili 125 katika eneo la mwezi kabla ya kurudi duniani. Hakueleza kiwango cha pesa ambacho wamelipa pamoja na mkewe, ingawa alisema kuna nafasi kumi ambazo zimebaki kwa watu wengine kujiunga nao.

Kwa upande wake, Maezawa amelipia viti vyote katika ziara yake inayoitwa "dearMoon", inayopangwa mapema mwaka ujao au baadaye kidogo.

Mnamo 2001, Tito alilipa Sh2 bilioni kuzuru Kituo cha Kimataifa cha Angani (ISS) akitumia roketi kutoka Urusi. Huo ulikuwa mwanzo wa binadamu wa kawaida kuzuru angani.

Kitaaluma, Tito ni mhandisi wa masuala ya angani, na alifanya kazi katika Maabara ya Kurusha Roketi katika Mamlaka ya Usafiri wa Angani ya Amerika (Nasa) miaka ya 1960. Baadaye, alifungua kampuni yake ya Wilshire Associates mnamo 1972.

Mkewe, Akiko, ni mhandisi wa mitambo. Alijitosa katika sekta ya fedha na kuhamia jijini New York, Amerika mnamo 1995. Akaeleza: "Nataka watu wajue wanaweza kutimiza lolote wanaloamini maishani. Hujachelewa hata kidogo, licha ya umri, asili wala jinsia."

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya afrika

■ WANAMGAMBO WAVURUGA AMANI BURKINA FASO

# URUSI ILIVYOSAIDIA MAPINDUZI



Kiongozi mpya wa Burkina Faso Kapteni Ibrahim Traore (wa pili kushoto) akifika kwa sherehe ya kuwakumbuka wanajeshi waliouawa katika eneo la Gaskinde, jijini Ouagadougou, mnamo Oktoba 8. Watu 37 wakiwemo wanajeshi 27 waliuawa katika shambulio la Gaskinde, lililotekelezwa na kundi la kigaidi la Al-Qaeda, mnamo Septemba -26.

*Prigozhin, mshirika wa karibu wa Rais Putin na mwanzilishi wa Wagner Group - shirika la kisiri la mamluki walio katika nchi kadhaa za Afrika - alimpongeza kiongozi kijana wa utawala wa kijeshi, Kapteni Traoré, akimtaja kuwa "mwana halisi na jasiri wa nchi yake"*

• OUAGADOUGOU

Katika mapinduzi ya hivi punde nchini Burkina Faso, vijana walionekana wakipeperusha bendera za Urusi kwenye barabara za jiji kuu, Ouagadougou, jambo ambalo lazima lilifurahisha Ikulu ya Kremlin ya Urusi.

Ingawa walikuwa wachache, wamezua uvumi kuwa huenda Urusi ilihusika katika matukio yaliyofanya Kapteni Ibrahim Traoré kutwaa mamlaka katika nchi hiyo iliyovurugwa na ongezeko la ghasia za wanamgambo.

Yevgeny Prigozhin, mshirika wa karibu wa Rais Putin na mwanzilishi wa Wagner Group – shirika la kisiri la mamluki walio katika nchi kadhaa za Afrika alimpongeza kiongozi kijana wa utawala wa kijeshi, Kapteni Traoré, akimtaja kuwa "mwana halisi na jasiri wa nchi yake".

"Raia wa Burkina Faso walikuwa chini ya minyororo ya wakoloni, waliokuwa wamepora watu na kuwachezea shere, walifunza, kusaidia magenge ya majangili na kusababishia watu wa nchi hiyo uchungu mwingi."

Hapa anazumzia Ufaransa, iliyotawala nchi hiyo enzi za ukoloni - na waliokaribisha mapinduzi katika nchi hiyo ya Afrika Magharibi, hawakupeperusha bendera za Urusi tu, bali pia walishambulia taasisi za Ufaransa, ukiwemo ubalozi.

Ghasia hizo zilizua hofu katika eneo hilo, kwa mara nyingine zikionyesha chuki kubwa dhidi Ufaransa katika zilizokuwa koloni zake Afrika.

Kwa karibu miaka kumi, Ufaransa imekuwa ikijaribu kusaidia majeshi ya nchi zilizo eneo la Sahel - ukanda kame kusini mwa Jangwa la Sahara, unaojumuisha Burkina Faso - kukabiliana na wanamgambo, baadhi yake wakishirikiana na al-Qaeda au kundi la the Islamic State.

Lakini majuzi iliondoka katika nchi jirani ya Mali, ambayo pia ilikuwa koloni yake, kufuatia kuvunjika kwa uhusiano na watawala wa kijeshi katika nchi hiyo, ambayo imekuwa iki-

...Endelea Uk 26

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Nia ya Urusi katika mapinduzi Burkina Faso

Kutoka Uk 25

laumiwa kwa kugeukia Urusi kwa misaada kupigana na wanamgambo.

Sergei Markov, ambaye alikuwa mshauri wa Urusi, ametoa kauli wazi: "Watu wetu walisaidia kiongozi mpya (wa Burkina Faso)."Nchi nyingine ya Afrika sasa itaacha kushirikiana na Ufaransa na kuwa mshirika wa Urusi."

Kwa mchanganuzi wa siasa, Dkt Samuel Ramani, hii inaashiria mwisho wa mbinu za kawaida za Urusi kwa machafuko ya kisiasa katika eneo hilo."Katika mapinduzi ya kijeshi yaliyotangulia, Urusi imekuwa ikijaribu kujionyesha kama inayonufaika kwa ajali tu na mabadiliko ya serikali," anasema Dkt Ramanai wa Royal United Services Institute (Rusi), taasisi ya masuala ya ulinzi na usalama, na mwandishi wa kitabu - Russia in Africa."Kwa wakati huu, Urusi inahusika zaidi na kuunga mkono mapinduzi hayo na hii imezua uvumi kuwa ilitekeleza jukumu la kuyashirikisha."

Inaaminika Urusi ilitumia Wagner Group, ingawa imekuwa ikikanusha mamluki hao wana uhusiano na serikali na hakuna ushahidi wa kuhusika moja kwa moja kwa Urusi. Punde tu baada ya kutwaa mamlaka, Kapteni Traoré alitangaza wazi kuwa alitaka kushirikiana na washirika wapya wa kimataifa kuwatimua wanamgambo wa Kiislamu ambao wamepiga kambi katika nchi hiyo tangu 2015.

Wengi walichukulia kuwa alimaanisha raia wa Urusi. Lakini lengo lake likiwa kuwashinda wanamgambo, anasema yuko tayari kushirikiana na Amerika au nchi nyingine iliyo tayari kusaidia kuimarisha usalama katika nchi hiyo. Amerika huandaa mafunzo makubwa ya kukabiliana na ugaidi kila mwaka kwa nchi za Afrika Magharibi - ingawa mwaka huu Mali na Burkina Faso hazikushiriki mafunzo hayo kwa jina Operation Flintlock.

"Nafikiri Burkina Faso inataka kuepuka mtego ambao Mali ilitumbukia," anasema Dkt Ramani, na kuongeza kuwa utawala wa kijeshi ulikuwa ukichukia sana raia wa Ulaya na Amerika tangu ulipotwaa mamlaka 2020."Kwa wakati huu wanategemea kikamilifu na wametekwa na serikali ya Urusi," anasema."Urusi ikiingia katika hali kama hii hawawezi kuiondoa. Hali kama hiyo ilikumba Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR)."

Wagner Group imekuwa ikiendeleza shughuli zake CAR tangu 2018 na wanachama wake wamelaumiwa kwa ukiukaji wa haki za binadamu, yakiwemo mauaji ya halaiki, kutoweka kwa watu na ubakaji. Ni vigumu kuchukulia hatua makundi kama Wagner, anasema Dkt Sorcha MacLeod, Profesa Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Copenhagen na mwenyekiti wa UN Working Group kuhusu Matumizi ya Mamluki.

"Ukiwa na mamluki hawa hapa, serikali inaweza kuhusika na mizozo ya kutumia silaha, bila kuwa mhusika rasmi wa mzozo huo. Kisha unaweza kuwa na sababu ya kukataa na hii ina athari kubwa kuhusu uwajibikaji."Kuwepo kwao pia kunaweza kuwa na athari mbaya, anasema.



Wafuasi wa kiongozi mpya wa Burkina Faso Ibrahim Traore wakibeba bendera za Burkina Faso na Urusi wakati wa maandamano karibu na makao makuu ya redio na televisheni ya kitaifa (RTB) jijini Ouagadougou mnamo Oktoba 6. Taarifa rasmi zinasema Kapteni Ibrahim Traore aliteuliwa rais wa Burkina Faso mnamo Oktoba 5, kufuatia mapinduzi ya pili chini ya miezi sita katika nchi hiyo ya Afrika Magharibi.

Amerika inakubaliana naye ikisema mamluki wa Urusi wanajifaidi na mali asili katika CAR, Mali na Sudan ili kufadhili vita vya Urusi nchini Ukraine.

Katika onyo kali wiki jana, balozi wa Amerika katika Umoja wa Mataifa alitaja hiyo kuwa gharama kubwa kwa Afrika."Badala ya kuwa mshirika wa kuimarisha usalama, Wagner hufyonza nchi wateja wake zinazolipia huduma za usalama kwa dhahabu, almasi mbao na mali asili nyingine - hii ni sehemu ya muundo wa biashara ya Wagner Group katika CAR," Linda Thomas-Greenfield akaambia kikao cha Usalama cha Umoja wa Mataifa.

"Tunajua mali hii inayopatikana kwa haramu inatumiwa kufadhili vita vya Urusi barani Afrika, Mashariki ya Kati na Ukraine."Haya yote yanaweza kuelezea kujikokota kwa Kapteni Traoré kutegemea Urusi pekee. "Nafikiri Traoré anajaribu kutazama mbele na kuonyesha anaweza kusawazisha pande zote," anasema Dkt Ramani."Lakini bila shaka ushirikiano wowote na Urusi utaondoa Ufaransa, na Amerika. Amerika na Ufaransa haziwezi kutangamana na Urusi."Je atashirikiana na Urusi kabisa? Au atatazama mbele na kujiweka katika hatari ya kukosa kuwa na mshirika halisi wa kigeni?"

Lakini hasira iliyoonyeshwa na vijana wa Burkina Faso inaonyesha ni lazima hatua ya kukabili magaidi ipewe umuhimu na kiongozi huyo mpya wa utawala wa kijeshi. Wiki hii, kiongozi mmoja wa eneo hili alisema Burkina Faso "imekuwa karibu kuporomoka" kwa kukosa usalama.

Hata hivyo, kuna maswali kuhusu jinsi wapiganaji wa Wagner wanaweza kufanikiwa Burkina Faso. Ingawa wamekuwa Mali kwa chini ya mwaka, dalili za mapema si nzuri kwa kuwa mashambulizi ya wanamgambo wa Kiislamu yameongezeka na wamelaumiwa kwa kukiuka haki za binadamu.

Nchi hiyo imekuwa kitovu cha mizozo katika ukanda wa Sahel, ikiwa na idadi kubwa ya mauaji kutokana na mashambulizi ya kigaidi kufikia sasa. Mwaka wa 2022 pia unatarajiwa kuwa hatari zaidi kwa Burkina Faso na Mali tangu maasi hayo yalipoanza."Wagner ni nzuri sana kwa kuzua ghasia. Lakini inashindwa katika mapigano hasa katika mazingira mageni na magumu," anasema Dkt Ramani.

Lakini anaamini tawala za kijeshi katika ukanda wa Sahel zitachagua kushirikiana na mamluki wa Urusi ikizingatiwa kuwa Ufaransa imeshindwa kukomesha kuenea kwa ghasia. Pia, Urusi ni mshirika wa kigeni asiye na matakwa mengi."Urusi inaonekana kuwa mshirika asiyehusika na haki za binadamu na demokrasia," anasema Dkt Ramani. "Aidha haijaribu kulazimisha mtindo wake wa maisha kwako - na hiyo inavutia madikteta na waporaji wa mali za nchi zao."

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya dunia

■ MZOZO KUHUSU UKRAINE: JINSI BIDEN ATARUSHA NUKLIA

# VITA VIKUU VYANUKIA



Rais wa Amerika Joe Biden (kulia) anasema Rais wa Urusi Vladimir Putin alifanya makosa makubwa kuanza vita na Ukraine.

*Rais wa Amerika anasema Putin anatisha ulimwengu na "vita vikuu" kwa kudokeza nia ya kutumia zana za kunuklia dhidi ya Ukraine. Amerika ikiingilia vita hivyo, mashambulizi yake yatatoka ndani ya gari rasmi la rais (the Beast), ndege ya Air Force One au ngome fulani ya kisiri.*

• LONDON

Huenda siku ya kiama ikaanza na mpira wa miguu - unaojulikana kama "mpira wa miguu wa kinuklia", mkoba fulani unaobebwa kila mahali anakoenda rais wa Amerika.

Mkoba huo mweusi uliojazwa vitu ndani, hauonekani kuwa chochiote, lakini umuhimu wake hutambuliwa kutokana na kuwa unabebwa na msaidizi wa rais aliyevalia mavazi ya kijeshi.

Ndani yake kuna vifaa vya kisiri vinavyomuwezesha rais kuamuru mashambulio ya kinuklia dhidi ya vituo fulani, popote ulimwenguni. Katika Ikulu ya White House, rais ana chumba maalumu ambako anaweza kutangaza vita na kuwasiliana na wakuu wa kijeshi.

Lakini wakati Rais Joe Biden, kwa mfano, alisafiri Puerto Rico, Florida, New York, New Jersey na Maryland mwezi huu wa Oktoba, alisafiri na "mpira wa miguu" wake jinsi tu anavyofanya akisafiri sehemu zingine.

Kulingana na Biden, Rais wa Urusi, Vladimir Putin anatisha ulimwengu kuwa kutatokea "vita vikuu" kwa kudokeza kuwa nchini yake inaweza kutumia silaha za kinuklia dhidi ya Ukraine. Amerika ikiingilia vita hivyo, mashambulizi yake yatatoka ndani ya gari rasmi la rais (the Beast), ndege rasmi ya rais, Air Force One au kituo fulani cha siri.

Raia wamewahi kupata nafasi ya kuona "mpira wa miguu" huo ambao unajulikana rasmi kama "Mkoba wa Dharura wa Rais," wakati fulani ulipopigwa picha ukibebwa nyuma ya aliyekuwa rais John F. Kennedy akiwa nyumbani kwake, Hyaniis Port, jimbo la Massachusetts mnamo 1963. Mwingine uliandama na Rais Ronald Reagan katika eneo la Red Square alipokutana Mikhail Gorbachev

Endelea Uk 28

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

# Ni hatua moja tu vita vya kinuklia vilipuke

Kutoka Uk 27

mnamo 1988.

Kifaa kingine cha siri, na muhimu, ambacho kinaweza kutumiwa kusababisha vita vya kinuklia kimepewa jina "biscuit" (biskuti). Kama "pira wa mguu" umebeba mipango ya kivita, "biskuti" inabeba nambari za kisiri ambazo rais anaweza kutumia kujitambulisha na kutoa amri.

Moja ya nambari hizo inafanana na kadi za kutoa pesa na hubebwa na rais kila wakati. Vifaa hivyo hubebwa chini ya ulinzi mkali na kwa usiri mkubwa.

Lakini nyakati zingine vifaa hivyo vimesababisha hali ya wasiwasi miongoni mwa walinzi wa marais wa Amerika.

Wakati mmoja ilidaiwa kuwa aliyekuwa rais Bill Clinton aliweka vibaya "biskuti" yake na kuibua wasiwasi miongoni mwa walinzi wake lakini baadaye ikapatikana. Rais Reagan pia aliweka kimakosa "biskuti" na nguo zake ndani ya mfuko wa plastiki akifanyiwa upasuaji hospitalini baada ya kupigwa risasi jijini Washington mnamo 1981.

Kundi la wafuasi wa Donald Trump lilipovamia majengo ya bunge katika jengo la Capitol mnamo Januari 6, 2021, ilimlazimu makamu wa rais Mike Pence kutoroka akiandamana na mlinzi wake aliyekuwa amebeba "mpira wa miguu" mbadala ambao pia huandamana na kila mrithi wa rais.



Wanajeshi wa nchi kavu wa Ukraine wakikabiliana na wanajeshi wa Urusi umbali wa mita 800 kutoka mstari wa mbele karibu na mji wa Toretsk, eneo la Donetsk, mnamo Oktoba 12, katika vita ambavyo vimetokana na Urusi kuvamia Ukraine.

Kuna utaratibu mrefu wa kufuata katika hatua ya kutangaza vita. "Rais wa Amerika ndiye pekee aliye na mamlaka ya kuagiza kuidhinisha matumizi ya silaha za kunuklia za Amerika," kulingana na Shirika la Utafiti katika Bunge la Congress (CRS).

Rais anatakiwa kujitambulishe kupitia nambari ya siri "biskuti" na pia atahitajika kujadili suala hilo na maafisa wa ngazi za juu katika jeshi.

Lakini licha ya marais "kuomba ushauri" kutoka kwa wakuu wa jeshi, "washauri hao wanahitajika kutekeleza amri hiyo ya matumizi ya silaha za kinuklia," inasema ripoti ya CRS. Amri hiyo itapitishwa kutoka safu ya juu hadi wanajeshi wa vyeo vya chini ambao husimamia hifadhi za silaha au mitambo ya kivita.

Hata hivyo, wanajeshi wa Amerika wanahitajika kukaidi amri ambazo zimetolewa kinyume cha sheria. Alivyosema John Hyten, aliyekuwa Kamanda wa Kikosi cha Mikakati (STRATCOM) nchini Amerika mnamo 2017: "Huwa tunafikiria zaidi kuhusu masuala kama haya" "Kama ni kinyume cha sheria, unajua nitakachosema, 'Bw Rais, hiyo ni kinyume cha sharia.' Naye atafanya nini? Atauliza, ni hatua gani inayokubalika kisheria?' Na tutamshauri kuhusu la kufanya ili kukabiliana na hali iliyopo. Inakuwa hivyo, si jambo gumu sana."

Hali ikiwa mbaya sana, baraza la mawaziri linaweza kuingilia kati na kumvua rais mamlaka yake, kwa kutumia marekebisho ya katiba nambari 25. Hali kama hiyo haijawahi kutokea, ingawa kuna madai kuwa suala hilo lilijadiliwa wakati wa utawala wa Trump.

Lakini kuna uwezekano kuwa mkondo wa kutoa maagizo unaweza kubadilika endapo rais amepangiwa kupewa huduma maalumu za kimatibabu.

Hali hii ilijiri mnamo Novemba 19, 2021, ambayo ilikuwa siku ya kihistoria: Biden alidungwa dawa ya kupoteza fahamu ili kufanyiwa upasuaji tumboni na makamu wa rais, Kamala Harris, akawa mwanamke wa kwanza nchini Amerika kuwa Amiri Jeshi Mkuu wa majeshi kwa dakika 85 akibeba "biskuti" na "mpira wa miguu"

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*



Wanajeshi wa Ukraine wakibeba silaha baada ya mashambulizi dhidi ya wanajeshi wa Urusi umbali wa mita 800 kutoka mstari wa mbele karibu na mji wa Toretsk, eneo la Donetsk, mnamo Oktoba 12, katika vita ambavyo vimetokana na Urusi kuvamia Ukraine.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

AJALI YA URUGUAY NA ULAJI NYAMA YA BINADAMU ULIOISHANGAZA DUNIA

# MUUJIZA WA ANDES

*Jinsi pekee ya kuishi ilikuwa kula nyama ya wafu. Lakini kwa Harley, mhandisi mstaafu aliye na umri wa miaka 70, hilo halikuwa tukio la kuogofya zaidi katika mkasa huo uliofanywa maarufu na sinema kwa jina "Hai" ya 1993.*

• MONTEVIDEO

Usiku wa kwanza ndio ulikuwa mbaya zaidi, Roy Harley amakumbuka wiki kumi ambazo yeye na manusura wengine wa ajali ya ndege miaka 50 iliyopita waliokoa maisha yao kwa kuning'inia kwenye barafu aina ya Andlean bila chakula au malazi, na sababu ndogo sana ya kuwa na matumaini.

Kati ya abiria 45 wa ndege hiyo, 16 walifika baada ya kuteseka kwa siku 72 katika kisa ambacho baadaye kiliitwa 'Muujiza wa Andes." Jinsi pekee ya kuishi ilikuwa kula nyama ya wafu. Lakini kwa Harley, mhandisi mstaafu ambaye sasa ana umri wa miaka 70, hilo halikuwa tukio la kuogofya zaidi katika mkasa huo uliofanywa maarufu na sinema kwa jina "Hai" ya 1993.

Baada ya mshtuko wa kwanza ndege iliponguka kwenye milima ya Andes siku ya Ijumaa, Oktoba 13, 1972, Harley na manusura wengine 31 walijipata eneo la giza juu ya mlima huku kiwango cha joto kikiwa chini ya nyuzi 30. Wengi wao wakiwa na chini ya miaka 20 – ndege hiyo ilikuwa ikisafirisha timu ya raga ya wachezaji chipukizi wa Uruguay na jamaa zao kwa mechi nchini Chile. Hakuna aliyevaa mavazi ya kujikinga na baridi.

Walilazimika kushikilia mabaki ya ndege hiyo, yaliyokuwa katikati ya miili ya waliofariki na waliojeruhiwa. "Usiku huo nilijipata Jehanamu," akasema Harley, akihojiwa na shirika la AFP.

"Miguuni mwangu, alikuwa mvulana aliyepoteza sehemu ya uso wake na…alikuwa akivuja damu nyingi. "Sikuwa na ujasiri wa kumshika mkono kumliwaza. Niliogopa. Niliogopa sana."

Asubuhi, watu wanne zaidi walikuwa wamefariki, na huo ukawa mwanzo wa mahangaiko ambayo hatimaye yalipunguza idadi ya manusura hadi 16 pekee. Kulikuwa hali nyingi za kuogofya. "Sina maneno ya kuelezea baridi ilivyojkuwa," akasema Carlos Paez, 68.

"Tuliumia kwa baridi, ilikuwa hali ngumu, hata sina maneno ya kuielezea," akaeleza. Mara nyingi walifikiri huo ulikuwa mwisho wao.

Siku ya 10, manusura hao walisikia kupitia redio ya ndege hiyo kuwa shughuli ya kuwatafuta ilikuwa imesitishwa. "Jambo moja lililonipa uchungu lilikuwa… kubaini kuwa dunia ilikuwa ikiendelea kama kawaida bila sisi," akasema Paez, ambaye sasa husafiri maeneo tofauti duniani kama mzungumzaji wa kuwapa watu matumaini maishani.

Lakini manusura walihitaji tangazo hilo ili kujitahidi kujaribu kujitoa juu ya barafu, akakumbuka, akakumbuka. Suala lingine ambalo ilikuwa shida kwao kuzungumzia ni ulaji wa nyama ya binadamu.

Hapakuwa chakula chochote katika ndege hiyo kwa kuwa safari ilikuwa fupi, kutoka Mendoza nchini Argentina ambako wasimama kwa muda hadi Santiago, nchini Chile.

Hapakuwa na chochote kinachoweza kuliwa katika eneo hilo lililofunikwa na barafu na muda si mrefu manusura waliumwa na njaa wasiyoweza kuvumilia.

Walikubaliana kwa pamoja kula nyama ya marafiki zao waliofariki. "Tulikuwa tumejaribu kula ngozi, tulijaribu kula sigara, tulijaribu kula dawa ya meno," akakumbuka Harley nyumbani kwa Paez, jijini Montevideo. "Tulikuwa tunakufa. Katika hali ya kuchagua kufa ama kula kitu pekee tulichokuwa nacho… tulifanya tulichoweza ili kuwa hai."

Katika siku ya 16, mkasa uliwafika tena. Barafu iliporomoka na kufunika mabaki ya ndege, mbayo yalikuwa nyumba yao. Walikuwa wamelala. Wanane kati yao walifariki, wakabakia 19 kati ya 32 wa awali. Wengine watatu walifariki baada ya siku kadhaa. "Ni kama Mungu alikuwa ametudunga kisu mgongoni kupitia poromoko hilo," akasema Paez.

Kwa kutumia ujuzi, bila vifaa vyovyote, manusura hao walijifunza kutumia mabaki ya ndege kuunda kofia za kujikinga na maporomoko zaidi, viatu ya kutembea kwenye barafu na miwani ya kujikinga na athari za barafu.


Mwishowe msaada ulifika. Katika juhudi ya mwisho, ambayo karibu iwaangamize, manusura Roberto Canessa na Fernado Parrado walitembea kwa siku kumi katika mazingira magumu na mageni.

Walifika kwenye mto na wakaona wanaume waliobebwa na farasi upande wa pili wa mto huo. Kutokana na kelele ya maji, sauti zao hazingesikika. Siku iliyofuata, mmoja wa wanaume hao alirudi na karatasi iliyofungiwa kwenye jiwe akawarushia

Kwenye karatasi hiyo, Parrado aliandika ujumbe wa kuomba msaada akisema: "Nimetoka katika ndege iliyoanguka kwenye milima." Siku iliyofuata, helikopta za kwanza zilifika.

Harley na Paez wanasisitiza kuwa wa si waathiriwa; simulizi yao ni kuhusu uvimilivu na ushirikiano. "Ni simulizi ya kipekee kuhusu watu wa kawaida," akasema Paez. "Mwishowe, uhai ulishinda."

*-Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*



Roy Harley, mmoja wa manusura one 16 wa ajali ya ndege eneo la Andes nchini Chile mnamo 1972 , akizungumza mjini Viñedos de la Tahona, jimbo la Canelones, nchini Uruguay, mnamo Agosti 15.

Nation Media Group "ePaper Copy"

TANZIA

PUMZIKA MAMLKANI

# VICHEKO VYA CHEPKUT VYAKOMA

*Ucheshi na unyenyekevu wa mbunge huyo wa zamani utakumbukwa na wengi. Tabia yake hiyo haikulenga kupata umaarufu wa kisiasa lakini kutangamana na wananchi wa kawaida waliompa nafasi ya kuwahudumia*

NA COLLINS OMULO

William Kamuren Chirchir Chepkut alikuwa mtu wa kipekee. Akiwa mchangamfu na mcheshi, Chepkut hangeweza kuelezewa kwa neon moja pekee.

Wakati ambao wenzake katika Bunge la Kitaifa walipata umaarufu kwa makosa yao, mbunge huyo wa zamani wa Ainabkoi alikuwa kipenzi cha wengi kutokana na unyenyekevu wake na uwezo wa kuvutia watu.

Alikuwa mtu mwenye sifa zilizokinzana, pia: nyingine zilionekana za mtu asiye muungwana. Alielezea hisia zake wazi bila kuficha lolote.

Daima, alivaa suti nadhifu chapa 'three-piece', lakini kwake, zilikuwa vilikuwa tu vipande vya nguo. Wakati mwingine alionekana akitumia upande wa ndani wa suti yake kupanguzia uso wake baada mlo katika hoteli ya Bunge.

Huyo ndiye Chepkut hasa. Hakuwa na mipaka na unyenyekevu wake ulikiuka tofauti za kitabaka au kikabila. Alitangamana na kila mtu, mahali popote, na mara nyingi alionekana akisaidia kupika wakati wa harusi, kuchimba makaburi ya waliofariki katika eneobunge lake, kucheza densi wakati wa hafla tofauti au akifurahia githeri pamoja na wahudumu wa matatu wakiandamana, bila kujali cheo chake cha "mheshimiwa."

Alikuwa mwepesi ya kuzua vitimbi na kuwavunja mbavu watu kwa kicheko hata nyakati zisizo za furaha. Kwake, hayo yote hayakulenga kupata umaarufu wa kisiasa, bali kutangamana na wananchi wa kawaida waliompa nafasi ya kuwahudumia.

"Mimi ni mzalendo na si mwanachama wa vikundi vidogo vya kikabila. Uongozi hutoka kwa Mungu. Kwa kutambua hilo, ni lazima tuwahudumie binadamu wenzetu kwa uungwana, hekima, usawa na haki. Lazima tuepuka tamaa na ubaraka," akasema.

Sifa na umaarufu wake zilitanda kutoka Kaunti ya Uasin Gishu, anakotoka, hadi jukwaa la kitaifa kupitia ushirikiano wake wa karibu na Nicholas Kipyator arap Biwott, aliyekuwa mshirika mkuu Rais Daniel arap Moi. Aliwa msaidizi wa kibinafsi wa Biwott alipokuwa Waziri katika Afisi ya Rais kati ya 1997 na 2003.

Chepkut hakuamini simu za mkononi na ilimchukua muda mrefu sana kumiliki moja. Kwenye hotuba yake ya mwisho katika Bunge, Chepkut aliwashauri wabunge wenzake wamwamini Mungu na kuokoka ili wapate nafasi ya kukutana na shujaa wake, Biwott. "Sote tutaenda mbinguni na kumpokea Rais Moi. Tutamuona Jomo Kenyatta, tutamuona shujaa wangu Nicholas Kipyator Kiprono Biwott na Jaramogi Oginga Odinga," akasema Chepkut, kauli iliyozua vicheko miongoni mwa wabunge wenzake.



William Chepkut

Uaminifu wake kwa Moi na Biwott haukuwa na doa. Moi alipofariki, Chepkut alimkashifu vikali mbunge mwenzake kwa kumkosoa Moi. "Moi alikuwa mtu mzuri. Wewe si Mungu kukosoa na huna uwezo wa kukosoa. Hakuna mtu mbaya kwa hii dunia," akasema.

Kila mara Chepkut aliposimama kuzungumza bungeni (mara 232), hotuba zake, ambazo ziliandama na ishara, ziliwavunja mbavu wenzake.

Chepkut aligombea ubunge eneo la Ainabkoi mnamo 2013 kwa chama cha National Vision Party (NVP) cha Bw Biwott, lakini akashindwa na Bw Samuel Chepkong'a wa chama cha United Republican Party (URP).

Walikabiliana tena 2017 Chepkut akiwa mgombeaji huru na akamshinda Chepkong'a wakati huo akigombea kwa chama cha Jubilee (JP). Chepkong'a alishinda kiti hicho tena katika uchaguzi wa Agosti 9, kupitia chama cha Rais William Ruto cha UDA.

"Mtu pekee aliye hai" kama alivyopenda kujiita kutokana na kunusurika kifo mara kadhaa, Chepkut alipumua mara ya mwisho Jumamosi, Oktoba 8, 2022.

Aliugua figo kwa muda mrefu, akiishi na figo moja aliyochangiwa na dada yake na akitibiwa kwa muda mrefu. Atazikwa Jumanne ijayo, Oktoba 18, nyumbani kwake eneo la Kapsundei, Kaunti ya Uasin Gishu.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep





**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE** SMS text and **FREE** Delivery

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*




ePaper Copy Nation Media Group ePaper Copy Nation Media Group ePaper Copy Nation Media Group ePaper Copy Nation Media